# Roho Mtakatifu Ni Nini?

. . .kwa ajili ya mkutano. Mkutano huu utakuwa tofauti kidogo na ile ya kawaida tunayokuwa nayo hapa. Kwa kawaida, kila wakati tunapokuja pamoja hapa, ni mkutano kwa wa. . .kwa ajili ya kuponya wagonjwa na kwa ajili ya mahitaji ya mwili. Mkazo unawekwa juu ya jambo hilo. Bali usiku wa leo tumeanzisha ufufuo huu kwa ajili ya kuponya nafsi, ro—roho ya mwanadamu.

Walakini, Bwana akipenda, Jumapili asubuhi kwenye shule ya Jumapili, Jumapili asubuhi tutakuwa na maombi kwa ajili ya wagonjwa na mstari wa kawaida wa kuponya, Jumapili asubuhi, Bwana akipenda. Na juma hili usiku tumekazwa kuzungumzia juu ya mambo ya Milele kwa ajili ya na—nafsi.

2 Naam, tunajua ya kwamba wakati mwi—mwili umeponywa, hilo hutufurahisha sisi sote, kwa maana tunajua ya kwamba bila shaka inaonyesha ya kwamba Mungu wetu huwaponya wagonjwa. Bali mtu huyo mgonjwa, kama wakiishi muda mrefu kutosha, labda watakuwa wagonjwa tena, labda washikwe na ugonjwa ule ule walioponywa, na jambo hilo haliondoi kuponya. Daktari atatoa dawa kwa ajili ya kuvimba kwa pafu, na labda siku mbili baadaye watakufa kwa kuvimba kwa pafu baada ya yeye kuwatangaza wana afya. Unarudi tena. Bali hiyo nafsi inapoponywa, basi unao, ndani yako, Uzima wa Milele.

3 Nami naamini ya kwamba tumekaribia sana Kuja kwa Bwana Yesu, hata inatupasa kufanya yote tuwezayo kumleta kila mtu kwenye Ufalme, na kuuleta Ufalme kwa watu, tupate kuponywa roho zetu. Ninaamini ya kwamba Mwili wa Yesu ndio mwili ulio mgonjwa sana nijuao; hiyo ni kusema, u—ule Mwili, Mwili wa kiroho wa Kristo duniani, ni mgonjwa sana.

4 Na sasa, hatukusudii kuwacheleweshа sana usiku, kwa sababu katika usiku wa kwanza hatuna nafasi ya kuketi marafiki wetu wapendwa. Tuko katika mradi wa kujenga kanisa jipya, maskani makubwa papa hapa kwenye ploti hizi, ama po pote pale Bwana atakapotuongoza; bali tujuavyo sisi, hapa.

5 Na sasa tumetangaza mkutano, Jumatano mpaka Jumapili. Lakini basi Jumapili, inakaribia likizo za Krismasi; bali ina-. . .wakati wo wote Bwana anapotuambia tukome, wakati utakuwa ndio huo. Hatujui vile matokeo yatakavyokuwa. Lakini tukiamini ya kwamba hawa jamaa hapa kwenye Maskani na makanisa tunayoshirikiana nayo, ambalo ni, moja ya hayo ni—ni Maskani ya Utakatifu kule Utica, ambayo Ndugu Graham Snelling ndiye mchungaji wake, na katika New Albany ambako Ndugu—Ndugu Junie Jackson ndiye mchungaji, na pia kule nje kwenye barabara kuu ambako ndugu Ruddell ndiye mchungaji.

Sisi na wao ni, makanisa yanayoshirikiana na Maskani haya, tunajaribu kuwaleta hao. . . watu wetu katika ushirika mzuri zaidi pamoja na Kristo. Hilo ndilo kusudi letu. Kwa hiyo nimechagua kusoma na kufundisha juu ya, kwa siku chache zifuatazo usiku. . .

6 Usiku wa leo nataka kuzungumzia juu ya somo la: *Roho Mtakatifu Ni Nini*? Halafu kesho usiku, ninataka kuhubiri juu ya: *Alitolewa Kwa Ajili Gani*? Kisha Ijumaa usiku. . . Na, kwa vinasasauti, sitaki huu unaswe Ijumaa usiku: *Je, Ninampokeaje Roho Mtakatifu*? na *Je, Ninajuaje Nikiwa Naye*? Kisha tutaacha tu, kisha tuone vile Bwana atakavyotuongoza, kwa ajili ya Jumamosi na Jumapili. Na Jumapili asubuhi, ibada ya kuponya, na ibada nyingine ya uijilisti Jumapili usiku.

7 Basi sasa tunataka kila mmoja ajue jambo hilo. . . Nami najua vinasasauti vinafanya kazi kwenye chumba cha nyuma, nasi tunataka kusema jambo hili. Kwa sababu, katika mikutano hii kama huu, ya kiijilisti, tuna watu kutoka madhehebu ya makanisa mbalimbali ambao wamefundishwa katika kiwango chao wenyewe cha imani, kila mmoja. Na hilo ni sawa. Sijataka kamwe kuwa na hatia ya kupanda farakano miongoni mwa ndugu. Na huko nje mikutanoni, ninahubiri tu juu ya Kweli kuu za kiijilisi za Maandiko, juu ya yale ndugu wanaoidhamini mikutano yangu wanaamini. Lakini, humu maskanini, na—nataka kuzungumzia juu ya yale tunayoamini. Kwa hiyo, kama—kama huelewi jambo hilo, ningefurahi sana kupata barua ndogo ama maandishi madogo kutoka kwako, kuniuliza swali la—la sababu ya sisi kuliamini namna hiyo. Nami ningefurahia kujaribu kulieleza vizuri niwezavyo.

8 Mwajua, kila kanisa, kama hamna fundisho, ninyi si kanisa. Inawabidi kuwa na msimamo, kanuni fulani mnazoshikilia. Na haidhuru mtu fulani anaweza kuwa ni mshirika wa nini ama ni wa madhehebu gani, kama mtu huyo amezaliwa kwa Roho wa Mungu, huyo ni ndugu yangu ama dada yangu, haidhuru. . . Tunaweza tusikubaliane katika mambo mengine, kama vile mashariki ilivyo mbali na magharibi, bali tungali tu ndugu. Nami nisingefanya kitu ila kujaribu kumsaidia ndugu huyo apate kutembea karibu, na vizuri kwa Kristo. Nami ninaamini Mkristo ye yote aliye halisi na wa kweli, angenifanyia jambo lile lile.

9 Naam, nimeyaomba maskani haya. . . Sasa, hatuingilii jambo hili kwa ajili mkutano tu wa muda mrefu, nataka kuingilia jambo hili, nami nawatakeni, na nimewaomba, kuteketeza kila daraja iliyo nyuma yenu, na kutubu kila dhambi, kwamba tunaingilia jambo hili pamoja na yote yaliyo mioyoni mwetu na maishani mwetu. Hatuna budi kuja hapa kwa kusudi moja tu la kuzifanya nafsi zetu tayari kwa ajili ya Kuja kwa Bwana, wala si kwa kusudi lingine lo lote. Na kama nilivyonena na kusema, ya kwamba labda wakati mwingine huenda

nikafundisha ama kusema kitu fulani ambacho huenda kikawa kinyume kidogo na yale mtu mwingine, jinsi wanavyoliamini. Mi—mimi si—sikuja kwa ajili ya ubishi, mnaona, ni—nilikuja . . . Tuko hapa kujifanya tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana. Nami nafikiri ya kwamba kundi hili ndogo . . .

10 Hapa nina ndugu waliotutembelea ninaowajua, kutoka mahali mbalimbali, nasi tunafurahi kuwa nao. Na hapana shaka ila kule nje kwenye kusanyiko kule, kuna wengine waliotoka nje ya mji, kutoka huko nje kwenye miji midogo iliyo karibu na hapa. Nasi tunashukuru kuwa pamoja nanyi, na tunawathamini sana, kama mnatupenda vizuri kutosha kuja kusikia mambo haya. Mungu . . . Naomba uchukue nyumbani, Ndugu yangu, Dada, akiba zilizo kuu sana Mungu anazoweza kumwaga ndani ya moyo wako, ndilo ombi langu.

11 Basi kwa maskani haya madogo, kwa kuwa ninaamini ya kwamba ni moja ya watu walio bora sana ninaoamini wako duniani, wanahudhuria maskani haya. Naam, sikusema watu "wote" walio bora sana. Nilisema baadhi ya watu walio bora sana duniani wanahudhuria maskani haya. Lakini kwa kuwa siku baada ya siku, tunaporudi, kutoka kwenye mkutano baada ya mkutano, ninaona haja kubwa ya maskani haya, haja kubwa kwake, na hiyo ni ya kujazwa, ama kuwekwa wakfu, maisha ya kindani, kutembea karibu na Mungu. Nami nimewaahidi kufanya jambo hili, kuhubiri Jumbe hizi kwa ajili yao. Nasi tunafurahi kuwaingiza ndani na kushiriki pamoja nasi kwenye Neno, tunapofundisha na kujaribu kufafanua.

12 Naam, siku za kwanza tatu usiku hatutakuwa tukichukua somo kuhubiria, bali kufundisha Ujumbe kutoka kwa Neno la Mungu.

Na sasa, kwa kuwa, nisingemuuliza mtu ye yote kufanya jambo lo lote ambalo nisingeweza kulifanya mimi mwenyewe. Na juma hili limekuwa Kalvari kamili kwangu mimi. Nimekuwa karibu sana ku—kuzirai, kama ninavyoweza kukuita, hata karibu kuingia kichaa. Bali nimejitolea kwa kila juhudi, na kila kitu nijuacho, kwa Bwana.

13 Juzi usiku, kidogo baada ya usiku wa manane, mimi pamoja na mke wangu, baada ya kuketi, tukiomba na kuzungumza na Bwana, kwenye kile kiti kidogo cha kuegemesha miguu katika . . . chumba chetu cha mbele, tukiwa na Biblia mbili zilizofunguliwa, tulijiweka wakfu upya kwa Mungu, kwa utumishi mkamilifu, ya kwamba tungetoa nia zetu, na kila kitu, na kila wazo baya, na kumtumikia Bwana Yesu.

Nami ninatumaini ya kwamba hiyo imekuwa ndiyo nia yenu, pia, ya kwamba mmefanya jambo lile lile. Ndipo tunapokuja usiku wa leo, tunakuja juu ya mahali patakatifu, miongoni mwa watu ambao wamekuwa wakiomba, na kufunga, na kutengeneza yote, na wakijifanya tayari kupokea kitu fulani kwa Mungu.

Nami najua ya kwamba yeye atakayekuja akiwa na njaa hatarudi akiwa na njaa, bali Mungu atamlisha kwa Chakula cha Uzima.

14 Naam, kabla hatujasoma kutoka kwa Kitabu Chake kitakatifu, na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi.

15 Bwana, tayari kumetolewa ombi mahali hapa usiku huu. Kumekuwa na. . . Nyimbo za Zayuni zimeimbwa na watoto Wako. Mioyo yao imeinuliwa juu. Nasi tumekuja hapa kujiweka wakfu Kwako, na kukuabudu Wewe kutoka kwenye kilindi cha nafsi yetu. Nasi tunakukumbusha jambo hili, Bwana, ambalo ulisema ulipoketi juu ya ule mlima na kuwafundisha wanafunzi Wako, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa." Uliliahidi jambo hilo, Bwana. Tunakuja usiku wa leo na mioyo iliyofunguliwa. Tunakuja, tukiwa na njaa na kiu, nasi tunajua Wewe utatimiza ahadi Yako.

16 Tunapojitahidi kufungua kurasa hizi takatifu za Biblia, kusoma kutoka Kwake yaliyomo, jalia Roho Mtakatifu ayachukue tu kwenye kila moyo. Pia jalia Mbegu hiyo ianguke kwenye imani yenye kina kirefu na yenye rotuba, ambayo italeta kila ahadi ambayo Neno limetoa. Tusikie, Bwana, na utusafishe, na utujaribu. Na iwapo kuna kitu cho chote kisicho safi kwetu, Bwana, dhambi yo yote isiyotubiwa, cho chote kisicho sawa, kifunue sasa hivi, Bwana, tutatembea moja kwa moja na kufanya jambo hilo, kwa kuwa tunatambua ya kwamba tunaishi katika vivuli vya Kuja kwa Bwana Yesu. Nasi tumekuja, Ee Mungu Mtakatifu, kwenye vivuli vya haki Ya—Yako usiku huu, nasi tunaomba tupate kujitolea upya, na kujiweka wakfu, na kujazwa kwa Roho Mtakatifu katika maisha yetu.

17 Tunapoona mioto ya ufufuo ikianza kufifia, jalia tutie kuni za Neno, ili kwamba ziwashe moto mpya, kusudi mioyo yetu ijae bidii. Tutakase, Bwana, kupitia Neno Lako la thamani, na Damu Yako, na neema Yako, tunakusihi. Na shukrani zote na sifa zitakuwa Zako. Ondoa udhalimu wote kutoka mioyoni mwetu. Tusafishe, Ee Bwana. Tupe mioyo misafi, na mikono misafi, na nia safi, ili kwamba tupate kuja katika madhabahu Yako, usiku baada ya usiku, tukifurahi na kujazwa na Roho Wako. Tunaomba jambo hili katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

18 Nataka kusoma Neno sasa hivi. Na huku. . . nawauliza mlete Biblia zenu, na penseli zenu, makaratasi yenu, kwa ajili ya Maandiko, kama mkitaka kufanya hivyo, lingekuwa jambo zuri sana. Basi sasa wakati mnapofungua sura ya 7 ya Mitume, kwanza; kujibu lile swali, ama kuanza katika kujibu lile swali, *Roho Mtakatifu Ni Nini*?

19 Hakuna kitu kitakachomshida Shetani, hakujakuwa na kitu duniani bado ambacho kingepata kumshida Shetani, kama Neno

la Mungu. Yesu alilitumia katika vita Vyake vikuu; Yeye alisema, "Imeandikwa . . ."

20 Basi asubuhi ya leo, nilipokuwa nikisikiliza, siku chache zilizopita, matangazo yaliyoonekana kana kwamba yanataka kusema kwamba uumbaji ulitokana tu na majivu yaliyovuma pamoja, na madini ya chumvi kiasi fulani, na kemikali chache za dunia, na jua lenye joto liliumba chembechembe ya uhai na kuuleta uhai. Ni upuzi jinsi gani! Wakati, jua litaua kila chembechembe ya uhai. Weka chembechembe hai huko nje juani, litaiua mara moja. Na hakuna kitu kama hicho; bali Shetani anajaribu kunipiga konde kwa jambo hilo. Na baada ya kumpeleka mtoto wangu Rebeka shuleni asubuni ya leo, nilipokuwa nikirudi, nilianza kufungulia redio tena; nami nikafikiri ningeingia kwenye upuzi huo tena, kwa hiyo nikaifunga tu.

Basi nilipokuwa nikipanda kwenda barabarani, Shetani aliniambia, akasema, "Unajua ya kwamba Mtu huyu unayemwita Yesu alikuwa tu mtu kama, siku moja katika siku Zake, kama Billy Graham ama Oral Roberts. Alikuwa tu mtu fulani ambaye wao walianza kuwafanya watu wachache kukutanika karibu Yake na kusema, Yeye ni Mtu mashuhuri, na baada ya kitambo kidogo akawa mkuu zaidi, kisha akawa mu—mungu kwao. Na sasa, jambo hilo limesambaa ulimwenguni kote, kwa kuwa amekufa, na ni hayo tu."

21 Nami nikawaza, "Jinsi ulivyo mwongo!" Ndipo nikageuka mara tu nilipokuwa nikivuka Barabara ya Graham. Nikasema, "Shetani, wewe unayezungumza na dhamira yangu, ningetaka kukuuliza mambo machache. Ni nani ambaye wale manabii wa Kiebrani walinena kwamba Yeye angekuja? Ni nani aliyekuwa Masihi mtiwa mafuta? Ni nini kilikuwa juu ya watu hao waliomwona Yeye hapo awali na kusema habari za maisha Yake, maelfu ya miaka kabla Yeye hajafika hapa? Ni nani aliyetabiri jambo hilo kwa usahihi kabisa? Na hapo alipokuja, wao walisema, 'Alihesabiwa pamoja na wakosaji,' Naye alihesabiwa. 'Alijeruhiwa kwa makosa yetu,' na alijeruhiwa. 'Alifanya kaburi Lake pamoja na matajiri, lakini Yeye angefufuka, siku ya tatu,' Naye akafufuka. Kisha aliahidi Roho Mtakatifu, nami ninaye Huyo. Kwa hiyo ni afadhali uliondokee jambo Hilo, kwa kuwa imeandikwa katika Neno, na kila Neno ni kweli." Ndipo akaondoka. Mpe tu Neno; hilo linatosha. Yeye hawezi kuvumilia Neno hilo, kwa kuwa limevuviwa.

Hebu tuanze kusoma usiku huu katika sura ya 7 ya Kitabu cha Matendo.

> *Kuhani Mkuu akasema, Je! Mambo hayo ndivyo yalivyo?*

*Naye akasema, Ndugu zangu na baba zangu, sikilizeni: Mungu wa utukufu alimtokea baba yetu Ibranimu, alipokuwa katika Mesopotamia, kabla hajakaa Harani,*

*Akamwambia, Toka katika nchi yako na katika jamaa zako, ukaende hata nchi nitakayokuonyesha.*

*Ndipo alipotoka katika nchi ya Wakaldayo, akakaa Harani, akatoka huko baada ya kufa babaye, Mungu akamhamisha mpaka nchi hii mnayokaa ninyi sasa.*

*Wala hakumpa urithi humu hata kiasi cha kuweka mguu; akaahidi kwamba atampa, iwe milki yake, na ya uzao wake baadye alipokuwa hana mtoto.*

*Mungu akanena hivi, ya kwamba wazao wake watakuwa wageni katika nchi ya watu wengine, nao watawafanya kuwa watumwa wao, na kuwatenda mabaya kwa muda wa miaka mia nne.*

*Na lile taifa watakaowafanya watumwa nitawahukumu mimi, alisema Mungu; na baada ya hayo watatoka, nao wataniabudu* katika nchi hii.

*Akampa agano la tohara; basi Ibrahimu akamzaa Isaka, akamtahiri siku ya nane. Isaka akamzaa Yakobo. Yakobo akawazaa wale kumi na wawili, wazee wetu.*

22 Juu ya mahali hapa, tunataka kuliendea somo, ambalo nafikiri ni somo muhimu sana la siku hii, juu ya: *Roho Mtakatifu Ni Nini*? Ni kitu gani? Na, sasa, sababu ya mimi kuchagua masomo haya ya mfululizo namna hii, huwezi kuja na kumpokea Roho Mtakatifu isipokuwa unajua Yeye ni nini. Nawe huwezi kumpokea, kama unajua Yeye ni nini, isipokuwa uamini umepewa Yeye, Naye ni kwa ajili yako. Pia, basi, huwezi kujua kama unaye, ama hunaye, isipokuwa unajua matokea Yeye anayoleta. Kwa hiyo kama unajua Yeye ni nini, na Yeye ni kwa ajili ya nani, na tendo Yeye analosababisha anapokuja, basi utajua ulichopata utakapompata Yeye. Mnaona? Hilo tu litatosha.

23 Ni kama tu nilivyokuwa nikizungumza na Ndugu Yetu Jeffries leo, naye akasema, "Ningetaka kuwa mkutanoni usiku huu, bali nitakuwa kule kesho usiku." Hakujua mkutano ulikuwa unaendelea, kwa sababu hatukuutangaza; papa hapa tu. Baadhi ya. . .Ndugu Leo na hao wengine waliwaandikia baadhi ya marafiki wetu na kuwaambia, nje ya mji. Vema, kwa sababu hatukuwa na nafasi.

24 Sasa nikasema, "Ndugu Jeffries, kama ulinituma nishuke niende nikafunge moja ya visima vyako vya mafuta, nami sikujua kitu juu yake, labda ningekilipua. Huenda nikaingiza ufunguo usio wake ama niwashe mtambo mwingine. Ingenibidi kujua jinsi ya kufanya jambo hilo kabla ya kulifanya."

Na hivyo ndivyo ilivyo katika kumpokea Roho Mtakatifu. Huna budi kujua unakuja kupata nini, na jinsi ya kumpokea Yeye, na Yeye ni Nini.

Basi, kwanza, Roho Mtakatifu amekwisha ahidiwa.

25 Tungeweza kuchukua majuma kumi na kamwe . . . kupitia tu juu ya ukingo wa somo hili, kwamba Roho Mtakatifu ni nini. Bali, jambo la kwanza, ninataka kuliendea vya kutosha tu kutoa muhitasari kila usiku, halafu nione usiku unaofuata kama kuna maswali yo yote.

26 Ni wangapi humu ndani hawajampokea Roho Mtakatifu, hawajabatizwa na Roho Mtakatifu? Inueni mikono yenu; unajua ya kwamba hujabatizwa. Angalieni tu hiyo mikono?

Sasa nataka kuzungumzia jambo Hilo, juu ya Roho Mtakatifu kuwa Ishara, kwa kuwa Yeye ni Ishara. Tunatambua ya kwamba, ya kwamba ahadi zote zimetolewa kwetu na . . . Ibrahimu alikuwa baba wa ile ahadi, kwa maana Mungu alitoa ile ahadi kwa Ibrahimu na kwa Mzao wake baada yake. Ile ahadi ilitolewa kwa "Ibrahimu na kwa Mzao wake. Na Ishara hii ni kwa watu wa agano.

27 Naam, kuna tofauti kubwa mno kati ya Mkristo tu na Mkristo aliyejazwa na Roho Mtakatifu. Na sasa tutapata jambo hili kutoka kwenye Maandiko, na kuliweka katika Maandiko kabisa. Kwanza, kuna Mkristo anayekiri kuwa Mkristo. Bali iwapo Mkristo huyu bado hajajazwa na Roho Mtakatifu, yeye yuko tu katika mwendeleo wa kuwa Mkristo. Mnaona? Yeye amekiri kuamini jambo Hilo; anafanya kazi kulifikia Hilo, bali Mungu bado hajampa Roho huyu, Roho Mtakatifu. Yeye bado hajafikia lile lengo pamoja na Mungu, ya kwamba Mungu ametambua jambo hilo.

28 Kwa maana, kwamba, Mungu alifanya ahadi na Ibrahimu, baada ya kumwita Ibrahimu, jambo ambalo ni mfano wa kumwita mwamini leo.

Yeye alimwita Ibrahimu, naye Ibrahimu akatoka katika nchi yake akaenda katika nchi ya ugeni, kukaa katikati ya wageni, na jambo hilo lilikuwa ni mfano wa wakati Mungu anapomwita mtu kuacha uchoyo wake, atubu dhambi zake. Yeye basi anatoka kwenye umati aliokuwa ndani yake, kuishi katika umati mpya, miongoni mwa watu wa tabaka mpya.

Halafu baada ya Mungu kuona kuwa Ibrahimu ni mwaminifu kwa ahadi alizompa Mungu, ya kwamba yeye angempata mtoto, na kupitia kwa mtoto huyu dunia nzima ingebarikiwa, ndipo Mungu alithibitisha imani yake kwa kumpa ishara, na ishara hiyo ilikuwa ni tohara. Nayo tohara ni mfano wa Roho Mtakatifu.

29 Aya zinazofuata tu za sura hii ambazo ndiyo kwanza tuzisome, kama mnataka kuliandika. Ndipo . . . Stefano alisema, katika aya ya 51:

> *Enyi wenye* shingo gumu . . . -*siotahiriwa mioyo wala masikio, sikuzote mnampinga Roho Mtakatifu; kama baba zenu walivyofanya, na ninyi ni vivyo hivyo.*

30 Tohara ni mfano wa Roho Mtakatifu. Naye Mungu alimpa Ibrahimu ishara ya to—tohara baada ya yeye kumkubali Mungu katika ahadi Yake na kutoka akaingia katika nchi ya ugeni. Mnaona? Ilikuwa ni ishara.

Basi watoto wake wote, na mzao wake baada yake, wanapaswa kuwa na ishara hii kwenye mwili wao, kwa sababu ndiyo iliyokuwa tofauti. Ilikuwa iwatenganishe na watu wengine wote, ishara hii ya tohara.

31 Basi hiyo ndiyo Mungu anayotumia leo. Ni ishara ya tohara ya moyo, Roho Mtakatifu, anayelifanya Kanisa la Mungu Kanisa lililotengwa na kanuni zingine zote za imani, imani na madhehebu. Wao wako katika kila namna ya madhehebu, bali bado wao ni watu waliotengwa. Hebu nizungumze na mtu fulani dakika mbili, ninaweza kukwambia kama amempokea Roho Mtakatifu ama la; nawe unaweza pia. Yeye huwatenga. Yeye ni alama. Yeye ni ishara. Naye Roho Mtakatifu ni ishara. Na ni . . .

Mtoto ye yote aliyekataa tohara katika Agano la Kale, ambayo ilikuwa ni mfano uliomtangulia Roho Mtakatifu, alikatiliwa mbali na watu. Asingekuwa na ushirika na kusanyiko lile lingine kama alikataa kutahiriwa.

Sasa linganisha jambo hilo na siku hizi. Mtu ambaye angekataa kuupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, hawezi kuwa na ushirika miongoni mwa wale ambao wana Roho Mtakatifu. Huwezi tu kufanya jambo hilo. Huna budi kuwa na asili. Kama vile, ni . . .

32 Mamangu pale alizoea kusema, "Kila ndege na wimbile." Vema, ni msemo wa kale, bali ni wa kweli. Huwaoni jiwa na kunguru wakifanya ushirika. Chakula chao ni tofauti. Tabia zao ni tofauti. Shauku zao ni tofauti.

Basi hivyo ndivyo ilivyo kati ya ulimwengu na Mkristo wakati *umetahiriwa* na Roho Mtakatifu, ambalo linamaanisha, "kukata mwili."

33 Tohara ingaliweza tu kuwa katika mwanamume. Bali kama mwanamke alikuwa amaeolewa na mwanamume, yeye alikuwa sehemu yake, alitahiriwa pamoja naye. Mnakumbuka, katika Timotheo, ambapo ilisema mle ndani, "Walakini ataokolewa kwa uzazi wake, kama akidumu katika imani na utakatifu pamoja na moyo wa kiasi."

34 Sasa, tohara. Unajua wakati yule . . . Sara alipocheka kwenye hema nyuma yake, kwa ajili ya ujumbe wa yule Malaika,

wakati aliposema, “Ibrahimu” bila kujua Yeye alikuwa ni nani, mgeni, “yuko wapi mkeo, Sara?” Yeye alijuaje kwamba alikuwa na mke?

35 Kama alivyosema Yesu, “Kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Kumbukeni, ishara hizo hazikutolewa kule Sodoma na Gomora, huko ulimwenguni, kati ya wanadini. Bali ilikuwa kwa Wateule, wale walioitwa watoke. Naye Ibrahimu aliitwa atoke. Nalo neno *kanisa* linamaanisha “walioitwa watoke; waliotengwa,” kama vile Ibrahimu alivyojitenga na alikuwa ametahiriwa.

Halafu wakati Sara alipochelea ule ujumbe wa Malaika, Mungu angalimuua papo hapo; bali asingalimsumbua Sara bila kumsumbua Ibrahimu, kwa maana wao walikuwa mmoja. Yeye alikuwa sehemu yake. Ninyi si wawili tena, bali ni mmoja.”

36 Kwa hiyo, tohara, Roho Mtakatifu leo hutahirisha moyo. Na ni ishara, ishara iliyotolewa.

Mtu fulani alisema hivi majuzi . . . Ninarudia tu jambo hili, si kama mzaha. Kwa maana, ni kweli, bali linasikika kama mzaha. Kama ninavyosema mara nyingi, hapa si mahali pa mizaha. Bali kulikuweko na maskini Mjerumani huko kwenye Pwani ya Magharibi, ambako tulikuwa juzi. Akampokea Roho Mtakatifu. Ndipo akashuka akaenda barabarani, naye angetembea hatua chache, kisha angeinua mikono yake na kunena kwa lugha. Ndipo angekimbia, naye angeruka, kisha angepiga makelele. Naye alikuwa kazini, akifanya namna hiyo, ndipo bosi wake akamwambia, “Umekuwa wapi?” Ni—ninapenda mahali hapo ambapo umekuwa. Yeye akasema, “Hapana budi ulikuwa kule chini miongoni mwa kundi lile na nati.”

Akasema, “Basi unafikiri wao ni nati?”

Akasema, “Bila shaka wao ni nati?”

37 Akasema, “Vema, Bwana asifiwe kwa ajili ya nati!” Kisha akasema, “Je! wajua? Nati hufanya kazi kubwa sana.” Akasema, “Kwa mfano, motokaa, hebu toa nati zote ndani yake, nawe huna kitu ila lundo la ‘skrepu.’” Kwa hiyo hilo ni karibu kweli.

38 Unakuwa tofauti sana wakati Roho Mtakatifu anakuja juu yako, hata wenye akili wa ulimwengu huu hawakupendi, nao wanakuonea, nao hawataki kuwa na uhusiano wo wote nawe, hata kidogo. Umezaliwa katika Ulimwengu mwingine. Wewe ni mgeni tu kama, mgeni mara kumi kuliko ungelikuwa, kama ungekwenda katika sehemu za mbali sana za misitu ya Afrika. Wewe ni tofauti wakati Roho Mtakatifu anapokuja, na ni ishara. Ni alama miongoni mwa watu.

39 Sasa, mnasema, “Basi, Ndugu Branham, ishara hiyo ya tohara ilitolewa kwa Ibrahimu?” Hiyo ni kweli. “Na kwa Mzao wake?” Naam.

40 Vema, sasa tutafungua Wagalatia, sura ya 3, aya ya 29, na tuone tu jinsi hii ingetumika kwetu. Wagalatia 3:29, na tuone tu jinsi tohara hii ingetumika kwa Mtaifa, kama sisi ni Mataifa; ambao, kwa uzazi wa kawaida ndivyo tulivyo.

Sasa, ya kwanza, nataka kusoma aya ya 16.

> *Basi ahadi* ilinenwa *kwa ibrahimu na mzao wake* (Ibrahimu na mzao wake!) *Hasemi, Kwa wazao,*. . .

Namna yo yote tu ya. . .kusema, "Loo, mimi ni wazao wa Ibrahimu pia." La! Kwa "Mzao." Mzao wa Ibrahimu!

> . . .Si *kwa wazao, kana kwamba ni wengi, bali kana kwamba ni mmoja, Kwa—Kwa* wao . . .*Kwa mzao wako, yaani, Kristo.*

41 Kristo alikuwa Mzao wa Ibrahimu. Mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—] Vema, sasa hebu tupate aya ya 28 na ya 29.

> *Hapana Myahudi wala Myunani.* Wala *hapana mtumwa wala huru.* Wala *hapana mtu mume wala mtu mke. Maana* sisi sote tumekuwa *mmoja katika Kristo Yesu.*
>
> *Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi.*

Tunakuwaje "Mzao wa Ibrahimu?" Kwa kuwa katika Kristo, ndipo sisi ni mzao wa Ibrahimu. Basi mzao wa Ibrahimu ulikuwa ni nini? Kama, tunaweza kwenda kwenye Warumi 4 na mahali mbalimbali.

Ibrahimu hakupokea ahadi kamwe wakati alipotahiriwa. Kuonyesha ya kwamba tohara ilikuwa tu ni mfano, yeye aliipokea ahadi *kabla* hajatahiriwa. Nayo ilikuwa ni mfano, wa kuitambua imani yake aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa.

42 Sasa, tunapokuwa katika Kristo, tunakuwa Mzao wa Ibrahimu na sisi ni warithi pamoja na Kristo, kwa hiyo, haidhuru sisi ni nani, Myahudi ama Mtaifa.

Naye, "Mzao wa Ibranimu," Mzao wa Ibrahimu ana imani ya Ibrahimu, ambaye humchukua Mungu katika Neno Lake. Haidhuru linaonekana la kipuzi namna gani, jinsi unavyotenda kigeni, jinsi Hilo linavyokufanya wa kipekee, mchukue Mungu katika Neno Lake, bila kujali cho chote kile.

43 Ibrahimu akiwa na umri wa miaka sabini na mitano, na Sara sitini na mitano, walimchukua Mungu katika Neno Lake, na kuita cho chote kilichokuwa dhidi Yake kama kwamba hakikuwa. Mnafikiri madaktari walifikiri nini, wa siku hizo? Unafikiri watu walifikiri nini, wakati walipomwona mzee, mwenye umri wa miaka sabini na mitano, akienda kila mahali akimsifu Mungu, yeye "atampata mtoto" kwa mkewe, naye huyo mwanamke akiwa na umri wa miaka sitini na mitano, kama

miaka ishirini na mitano baada ya kuingia ugumba? Lakini, mnaona, inakufanya utende kimzaha, ile imani ya Ibrahimu.

44 Basi wakati unapotahiriwa na Roho Mtakatifu, Huyo anafanya jambo lilo hilo kwako. Anakufanya ufanye mambo ambayo hukufikiri ungeyafanya. Anakufanya uchukue ahadi ya Mungu na kumwamini Mungu.

45 Naam, pia Yeye, mbali na a—ahadi na ishara, Yeye ni Muhuri pia. Sasa kama utaenda pamoja nami katika Warumi. Kwanza, ninataka uende pamoja nami kwenye Waefeso 4:30, na hebu tusome hapa kwa muda kidogo tu. Waefeso 4:30 inasema hivi.

Sasa, mmewasikia watu wengi sana wakisema ya kwamba vitu mbalimbali ni muhuri. "Kama ukiingia kanisani, una muhuri wa hilo kanisa." Halafu watu wengine wanasema, "Ni kuadhimisha siku fulani, siku ya Sabato, "hiyo—hiyo ndiyo muhuri ya Mungu." Baadhi yao husema, "Kama tukiweka ufuasi wetu katika madhehebu fulani, tumetiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu."

46 Sasa, Biblia ilisema, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na la Mungu liwe Kweli." Sasa Waefeso 4:30 inasema hivi:

> *Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi*."

47 Sina budi kusisitiza jambo hili kidogo sasa, kulieleza wazi. Sasa, enyi ndugu wa kisheria, tulieni tu kwa muda kidogo. Mnaona? Mliona huo muhuri unadumu muda gani? Si hata ufufo unaofuata, mpaka wakati mwingine kitu fulani kitakapoenda kombo. "Hata siku ya ukombozi wenu," huo ndio muda wewe uliotiwa muhuri. "Hata siku ya ukombozi wako," wakati utakapokombolewa kuwa pamoja na Mungu, huo ndio muda ambao Roho Mtakatifu anakutia muhuri. Si kutoka ufufuo hata ufufuo; bali kutoka Umilele hata Umilele, umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu.

Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, Yeye ni Muhuri wa Mungu, ya kwamba umepata . . . umepata neema mbele ya macho Yake, Naye anakupenda, Naye anakuamini, Naye ameweka muhuri Wake juu yako. Muhuri ni nini, mtu ye yote? Mbona, *muhuri* unaonyesha ama unamaanisha "kazi iliyomalizika." Amina! Mungu amekuokoa, akakutakasa, akakuosha, ukapata kibali Kwake, kisha akakutia muhuri. Yeye amemaliza. Wewe ni bidhaa Yake hata siku ya ukombozi wako. Kilichotiwa muhuri ni "kitu kimekamilika."

Roho Mtakatifu ni nini? Ni ishara. Tutaingilia jambo hilo baadaye kidogo, katika Ujumbe mwingine, ile ishara ambayo Paulo alinena habari zake. Lugha ilikuwa ni ishara kwa waamini . . . ama wasioamini.

48 Sasa angalieni, bali katika jambo hili, Roho Mtakatifu ni Ishara. Ninamaanisha…Na Roho Mtakatifu ni muhuri. Ni Ishara ambayo Mungu aliwapa watoto Wake waliochaguliwa. Kuikataa ni kukatiliwa mbali na watu; na kuipokea Hiyo, ni kumaliza na ulimwengu na mambo yote ya ulimwengu, na kuwa bidhaa ambayo Mungu ametia Muhuri wa kibali juu yake.

49 Nilikuwa nikifanya kazi katika reli huku nje pamoja na Harry Waterberry, nasi tungeshuka tukaenda kuipakia behewa. Ndugu yangu, "Doc," anayesimama kule nyuma, husaidia kupakia mabehewa. Wakati behewa linapakiwa, wao wanalikagua behewa hilo, mkaguzi, na kama akipata cho chote kilicholegea, ambacho kingeanguka na kuvunjika, ama kitu cho chote ambacho kingeharibu; yeye hatalitia muhuri behewa hilo mpaka behewa hilo limepakiwa kabisa, mpaka limeshindiliwa kabisa na ni sawa kabisa, hata kule kutikisa kwa safari hakutaidhuru bidhaa iliyo ndani.

50 Hiyo ndiyo sababu hatutiwi muhuri sana; tumelegea sana juu ya mambo. Wakati Mkaguzi anapoingia ndani, kuyakagua maisha yako, kuona kana kwamba wewe si mlegevu kidogo kuhusu mambo, mlegevu kidogo juu ya maisha yako ya maombi, mlegevu kidogo juu ya hasira hiyo, mlegevu kidogo juu ya ulimi huo, kuzungumza juu ya wengine, Yeye kamwe hatalitia muhuri behewa hilo. Tabia fulani chafu, vitu fulani vichafu, nia fulani ya ushenzi, Yeye hawezi kulitia muhuri behewa hilo.

Bali wakati anapopata kila kitu mahali pake, yule Mkaguzi, basi analitia muhuri. Mtu ye yote asithubutu kufungua muhuri huo mpaka behewa hilo limefika kikomo chake ambacho limetiliwa muhuri! Hilo hapo. "Msiwaguse masihi Wangu; msiwadhuru manabii Wangu. Kwa maana nawaambieni, ingekuwa radhi kwako jiwe la kusagia kuweka shingoni mwako, na utumbukizwe kwenye kilindi cha bahari, kuliko kujaribu kumuudhi ama kumtikisa kidogo aliye mdogo sana wa hawa ambao wametiwa muhuri." Mnaona kile linachomaanisha?

51 Hicho ndicho Roho Mtakatifu alicho. Yeye ni dhamana yako. Yeye ni Kinga yako. Yeye ni ushuhuda wako. Yeye ni Muhuri yako. Yeye ni Ishara yako, ya kwamba, "Mimi ninaelekea Mbinguni. Sijali anayosema ibilisi! Mimi ninaelekea Mbinguni. Kwa nini? Yeye alinitia muhuri. Yeye alinipa Huyo. Alinitia Muhuri katika Ufalme Wake, nami ninaelekea Utukufuni! Acha upepo uvume, acha Shetani afanye anachotaka. Mungu tayari amenitia muhuri hata siku ya ukombozi wangu." Amina! Hicho ndicho alicho Roho Mtakatifu. Loo, unapaswa kumtaka Huyo. Nisingeweza kuendelea bila Yeye. Mengi sana yangeweza kusemwa hapo, bali nina hakika mnajua ninalozungumzia.

52 Naam, pia, hebu tufungue Yohana 14, kwa muda kidogo tu. Ninapenda Neno sana! Ndilo Kweli.

53 Naam, Roho wa Mungu, Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu ni nini? Ni Roho wa Kristo ndani yako. Basi, kabla hatujasoma, ningetaka tu kutamka maneno machache hapa ya kuelezea. Roho Mtakatifu ni nini? Ni muhuri. Roho Mtakatifu ni nini? Ni Agano. Roho Mtakatifu ni nini? Ni Ishara. Roho Mtakatifu ni nini basi? Ni. . .Roho wa Yesu Kristo ndani yako. Mnaona? "Kitambo kidogo," kasema Yesu, "na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Roho wa Mungu katika Kanisa Lake!

54 Kwa ajili gani? Alifanya jambo hilo kwa sababu gani? Kidogo hili ni juu ya somo la usiku wa kesho. Lakini Yeye alifanya jambo hilo kwa sababu gani? Kwa nini Yeye, kwa nini Roho Mtakatifu. . .Yeye alikuja kwa, kwa ajili gani? Aliingia ndani yako kwa sababu gani, aliingia ndani yangu kwa sababu gani? Ilikuwa kwa ajili ya kuendeleza kazi za Mungu.

55 "Daima ninafanya jambo lile linalomfurahisha Baba Yangu. Sikuja kufanya mapenzi Yangu, bali ya Baba aliyenipeleka. Na Baba aliyenipeleka yuko pamoja Nami; na kama vile Baba Yangu alivyonipeleka Mimi, Nami nawapeleka vile vile." Loo, jamani! [Ndugu Branham anapiga makofi yake mara mbili—Mh.] Baba alimpeleka, alienda akiwa ndani Yake. Baba aliyempeleka Yesu Kristo alikuja ndani Yake, akafanya kazi kupitia Kwake.

Yesu anayekupeleka, huenda pamoja nawe na yuko ndani yako. Basi kama Roho huyo, aliyeishi katika Yesu Kristo, alimfanya afanye na kutenda jinsi alivyotenda, utakuwa na dokezo jinsi Yeye atakavyofanya akiwa ndani yako; maana Uzima huo hauwezi kubadilika. Utaenda kutoka mwili mmoja uingie mwingine, bali hauwezi kubadilisha tabia Yake, kwa maana Huo ni Mungu.

56 Sasa katika Yohana 14, hebu tu tusome kidogo tu, kuanzia aya ya 10:

> *Husadiki. . .kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu?* Zile kazi—*hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake.* (Wazieni jambo hilo sasa.)
>
> *Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe.*
>
> *Amin, amin, nawaambieni, Yeye aniaminiye mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye. . .; naaam, na kubwa kuliko hizi atafanya, kwa kuwa mimi naenda kwa Baba.*

Hamuoni? Mnaona jinsi alivyosema pale? Sasa angalia jinsi hili, jinsi jambo hili linatokea. Nitasoma mbele kidogo tu. Tutaendelea kusoma mpaka kama aya ya 20. "Nanyi mkiomba lo lote. . ." Hebu tuone, nilikuwa na. . .Naam! a-ha. Vema.

*Nanyi mikiomba lo lote kwa jina langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana.*

*Mkiomba neno lo lote kwa jina langu, nitalifanya.*

*Mkinipenda, mtazishika amri zangu.*

*Nami nitamwomba Baba*, (Sasa angalieni!) *naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele;*

*Ndiye Roho wa kweli; ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui; bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu, naye atakuwa ndani yenu.*

57 Roho huyo ni nani basi? Roho Mtakatifu ni nini? Ni Kristo ndani yako, yule Msaidizi; huyo ni Roho Mtakatifu. "Na wakati yule Msaidizi atakapokuja, atafanya mambo yale yale niyafanyayo Mimi wakati Msaidizi yu ndani Yangu. Nitamwomba Baba, Naye atawapelekea Msaidizi huyu. Mnamjua huyo Msaidizi. Ulimwengu haumjui, hautamjua kamwe. Bali ninyi mnamjua kwa sababu Yeye anakaa sasa pamoja nanyi," Yesu akinena, "bali Yeye atakuwa ndani yenu." Haya basi; huyo ndiye yule Msaidizi, "atakuwa ndani yenu."

*Sitawaacha ninyi yatima; naja kwenu.*

"Sita-. . ." Naam, huyo ni Msaidizi, Kristo. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo; ni Kristo.

*Bado kitambo kidogo na ulimwengu haunioni tena; bali ninyi* mtaniona. *Na kwa sababu mimi ni hai, ninyi nanyi. . .hai.*

58 Loo, tungeweza kuendelea na kuendelea; bali, kuwafanya mjue. Yeye ni nini? Yeye ni muhuri. Yeye ni ishara. Yeye ni Msaidizi. Angalieni yote aliyo Yeye. Mzao wa Ibrahimu humrithi Huyo.

59 Naam hebu pia tuone kwamba kile. . .ni kitu gani kingine alicho Msaidizi. Hebu tufungue Yohana wa Kwanza 16:7, tuone kama Yeye si Mwombezi, pia. Mnajua mwombezi ni nini, kumfanya mwombezi. Tuna Mwombezi. Tunajua jambo hilo. Yohana wa Kwanza sura ya 16. . . Loo, ngojeni kidogo, samahani. Yohana Mtakatifu, ndiyo, 16:7. Samahami. Hakika nasikitika sana nilisema jambo hilo. Nilisoma hilo vibaya kwenye nini hii yangu. . .nina 16:7

*Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi niondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu.*

*Naye akiisha kuja, huyo atauhakikisha ulimwengu kwa habari ya dhambi, na haki, na hukumu.*

*Kwa habari ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi;*

*Kwa habari ya haki, kwa sababu mimi naenda zangu kwa Baba, wala hamnioni tena;*

*Kwa habari ya hukumu, kwa sababu yule mkuu wa ulimwengu huu amekwisha kuhukumiwa.*

60 Jamani! Naam, Mwombezi anapatikana, katika—katika Yohana wa Kwanza 2:12. Sasa hebu tusome hilo, kwa muda kidogo tu, Yohana wa Kwanza 2:12. Samahani, Yohana wa Kwanza . . . 1 na 2, ndiyo hiyo. Nimeandika hivi, I Yonana 2:1-2

*Watoto wangu wadogo, nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mkitenda dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki,*

Mwombezi ni nani? Yesu Kristo, mwenye haki.

*Naye ndiye—ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwegnu wote.*

61 Roho Mtakatifu ni nini? Ni Mwombezi. Mwombezi . . . Mwombezi ni nini? Anafanya nini? Kufanya mwombezi? Ana rehema. Yeye, Yeye anasimama mahali pako. Yeye, Yeye anafanya mambo usiyoweza kufanya. Yeye, Yeye—Yeye ni kipatanisho kwa ajili ya dhambi zako. Ndiye haki yako. Ndiye kupona kwako. Ndiye Uzima wako. Ndiye kufufuka kwako. Yeye ni yote aliyo nayo Mungu kwa ajili yako. Yeye ni Mwombezi.

62 Jinsi tungaliweza kuingia kirefu juu ya jambo hilo na kulifafanua, na jinsi ambavyo wakati Yeye—Yeye anafanya maombezi kwa ujinga wetu. Wakati mwingine wakati yule . . . tunapompata Roho Mtakatifu, tunayumbayumba kijinga tukaingia ndani ya kitu fulani. Roho Mtakatifu yuko hapo kutufanyia uombezi. Yeye ni Mwombezi wetu. Anasimama pale . . . Yeye ni Wakili wetu. Anasimama pale na kututetea. Hatujitetei wenyewe, kwa maana Roho Mtakatifu ndani yetu hututetea. Roho Mtakatifu akitujalia kutamka, wakati mwingine kwa maneno huwezi kufahamu, naye anatuombea. Hicho ndicho alicho Roho Mtakatifu.

63 Ninatembea nikaingia katika jambo lo lote, ni—ninatembea kama mtoto mchanga; unatembea kama jamaa mdogo. Sisi, sisi tunatembea katika ulimwengu wenye giza uliojaa maadui, uliojaa dhambi, uliojaa mitego, uliojaa kila kitu.

Mnasema, "Loo, ninaogopa. Ninaogopa kuchukua maisha ya Mkristo. Ni, ninaogopa kufanya jambo *hili*. Ninaogopa kufanya jambo *hili*."

Usiogope. Tuna Mwombezi! Amina! Loo, Yeye anasimama karibu nasi. Yeye yuko ndani yetu, naye anatuombea! Roho Mtakatifu, daima, daima akituombea, wakati wote. Yeye ndiye Mwombezi wetu. Loo, jinsi tunavyomshukuru Mungu kwa jambo hilo!

64 Muhuri, ishara, Roho wa Uzima, Mungu wa Mbinguni, Msaidizi, Uzima, Mwombezi. Yeye ni nini! Loo, jamani! Tungeweza kuendelea kwa masaa kadha na jambo hilo.

65 Sasa tutabadilisha kwa muda kidogo tu. Sasa tutauliza sasa . . .

Tuliahidiwa katika siku za mwisho! Mwombezi huyu, muhuri, ahadi, kila kitu ambacho tumezungumza habari Zake usiku huu, pamoja na elfu kumi zaidi, Yeye alifanywa ahadi kwetu katika siku za mwisho.

Wao hawakuwa Naye siku hiyo. Wao walikuwa tu na muhuri katika mwili wao, kama ishara na dalili, wakiamini Yeye alikuwa anakuja, nao walitembea kwa kivuli cha torati. Ambapo, wao walitahiriwa kimwili.

66 Siku hizi sisi hatutembei kwa kivuli cha torati. tunatembea kwa nguvu za ufufuo. Tunatembea kwa nguvu za Roho, Ambaye ndiye Mhuhuri wetu wa kweli, Mwombezi wetu wa kweli, Msaidizi wetu wa kweli, ishara yetu ya kweli kwamba tumezaliwa kutoka juu; watu wa kigeni, wa kipekee, wanaotenda kiajabu, wakimchukua Mungu kwa Neno Lake, wakiita vitu vingine vyote kuwa si kweli. Neno la Mungu ni kweli. Hiyo . . . Loo, jamani! Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo.

67 Unamtaka Huyo? Hivi si ungetaka kuwa Naye? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hebu tuone kama aliahidiwa.

Sasa hebu turudi katika Isaya, Kitabu cha Isaya. Hebu tufungue sura ya 28 ya Isaya. Sasa tunaenda kwa Isaya 28, nasi tutaanzia yapata . . . Hebu tuchukue aya ya 8, tuone kile alichosema Isaya, miaka mia saba na kumi na mbili kabla Yeye hajakuja.

68 Tungeweza kusema mengi sana kuhusu jambo hili, turudi, huko nyuma kabisa, lakini tutaanzia papa hapa tuone kama Yeye aliahidiwa kwa Kanisa. Yeye alipaswa kuja siku gani? Kwenye siku za mwisho, wakati kungekuwako na u—u—potovu. Sasa kumbukeni, neno hilo liko katika wingi, "siku," siku mbili za mwisho, miaka elfu mbili ya mwisho.

Sasa, sasa aya ya 8:

> Zote, *maana meza zote zimejaa . . . uchafu, hapana mahali* pasafi.

69 Tafuta kila mahali leo upapate. Angalia kila mahali uone kama tuko katika siku hiyo. "Meza zote!" Mbona, wao wanaenda kwenye Meza ya Bwana, na kitu cha kwanza, katika vitu vya kawaida, wanachukua kipande cha kale cha mkate mwembamba ama biskuti ya soda, na kukivunja na kufanya ushirika. Wakati, huo unapaswa kuokwa kwa mikono yenye Roho Mtakatifu, na mkate usiotiwa chachu. Kristo si mchafu na mwenye unajisi, na huo unamwakilisha Yeye.

70 Jambo jingine, wao wanawapa watu wanaokunywa pombe, wanaodanganya, wanaoiba, wanaovuta sigara, wanaotafuna, (whiu!) cho chote kile tu, mradi tu wao ni wafuasi wa kanisa. Na iwe mbali! Kama mtu akiuchukua wakati tunaula huu hapa, yeye anavuta na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua Mwili wa Bwana. Iwapo yeye hayaishi yale maisha, usiukaribie.

Na kama huuli, inaonyesha ya kwamba dhamira yako mwenyewe ina hatia. "Yeye asiyeula, hana sehemu pamoja Nami," Yesu alisema.

71 Bali meza zote za Bwana zimejaa uchafu. Hakuna mahali hata pamoja palipo pasafi. Sikizeni, kama jambo hilo halionyeshi siku hizi!

> *Atamfundisha*. . .atafundisha *nani maarifa? atamfaha-. . . atamfahamisha nami habari hii?*. . .

> . . .ni nani atakayefahamu *maarifa*?. . . ni nani yeye anaweza kumfahamisha *habari hii*?. . .

"Vema, Mungu abarikiwe, mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mpetekoste. Mimi ni Mnazarayo. Mimi ni Mprigrim Holiness!" Hilo halimaanishi kitu kwa Mungu; ni meza nyingine tu.

> . . .ni nani nitakayemfahamisha *habari hii*?. . .

72 Ni habari za namna gani; Kimethodisti, Kibatisti, Kipresbiteri, Kipentekoste? Habari za Biblia!

> . . .ni nani nitakayemfahamisha *habari hii?* . . .

73 Unajuaje unapompokea? Tutaingilia jambo hilo Ijumaa usiku. Mnaona?

> . . .nitamfahamisha nani *habari hii?* (sasa angalia.) *wale walioachishwa maziwa, walioondolewa matitini.*

74 Watoto wachanga wanasema, "Vema, ninaenda kanisani, mamangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili." Sina kitu dhidi ya jambo hilo, ndugu mpendwa. Nami ninatambua huu unanaswa. Hilo ni sawa, kuwa mfuasi wa kanisa la mama. Lakini, sikiliza, mama alitembea katika nuru moja, unatembea katika nyingine.

75 Luther alitembea katika Nuru moja; Wesley alitembea katika nyingine. Wesley alitembea katika nuru moja; Pentekoste ilitembea katika nyingine. Lakini sisi tunatembea juu zaidi ya hiyo leo. Na kama kuna kizazi kingine, kitaenda juu kuliko sisi.

76 Huko nyuma katika siku za mwanzoni, wakati kitu hicho kilikuwa kipana, kipana sana, Luther alifundihsa Kuhesabiwa haki kwa imani. Hilo lilikuwa tu la kuwaleta watu kutoka Ukatoliki waingie Uprotestanti, waingie katika ushirika wa Neno. Kuhesabiwa haki kwa imani, hiyo ilikuwa duara kubwa na pana. Wao hawakutoka humo kamwe.

77 Hatimaye ukaja ufufuo mwingine ulioitwa John Wesley. Uliwatikisa wakashuka kutoka kwenye huo, na ukalitelemsha kwenye Utakaso, ishi. . .maisha mazuri, masafi, matakatifu, yaliyotakaswa na Neno la Mungu, yakupe furaha moyoni mwako. Huo ulitikisa ukaangusha mafundisho mengi ya Kiluteri.

78 Ndipo ikaja Pentekoste pamoja na Ubatizo wa Roho Mtakatifu, na kuupunguza upana wake tena, kwa kumpokea Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli.

Na sasa hiyo imeanza kutikisika ikaanguka. Na zile karama, na kule kurudishwa, na Roho wa Mungu ameingia, katika utimilifu wa ishara na maajabu, Kanisani, na kuitikisa Pentekoste. Ni nini? Tuko karibu sana na kule kuja kwa Bwana Yesu, hata Roho yule yule aliyekuwa ndani Yake anafanya kazi katika Kanisa, akifanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani. Jambo hilo halijakuwa mahali po pote, kutoka huko nyuma kwenye wakati wa mitume hata wakati huu.

Kwa nini? Mnaona? Ni pana; inapungua, inapungua, inapungua. Ni nini? Ni kama tu mkono wako ukifanyika kivuli; ile negativu, negativu, negativu. Lakini ni nini? Ni kurudisha nuru. Luther alikuwa nini? Kurudishwa kwa mfano wa Kristo. Wesley alikuwa nini? Kurudishwa kwa mfano wa Kristo.

79 Angalia, wakati wa Billy Sunday ndiyo kwanza umalizike. Juzijuzi, mzee Dk. Whitney, yeye amefundisha papa hapa kwenye mimbara hii, wa mwisho wa ile itikadi ya kale, alikufa, akiwa na umri wa karibu miaka tisini, nakisia. Billy Sunday alikuwa mfufuzi kwa makanisa ya kawaida ya siku zake. Yeye hakucheza; alisimama pale na kupaza sauti, "Enyi Wamethodisti wote, elekeeni kwa ule mburuzo wa unga wa mbao, wahubiri na kila mtu! Enyi Wabatisti wote elekeeni kwenye ule mburuzo wa unga wa mbao! Enyi Wapresbiteri!" Yeye hakucheza. Alikuwa Billy Graham wa siku hizi.

80 Angalia. Halafu, wakati ule ule ambapo kanisa la kawaida lilikuwa likipata ufufuo wao, nini kilichotukia? Injili Yote ilikuwa ikipata ufufuo. Wakatokea ndugu wa akina Bosworth, Smith Wigglesworth, na Dk. Price, Aimee McPherson, na wote hao.

Angalia, Smith Wigglesworth alikufa usiku mmoja. Dk. Price akafa asubuhi iliyofuata. Katika masaa ishirini na manne nilikuwa uwanjani.

81 Sasa mwisho wangu unakuja. Angalia kwenye. . .Hamsikii mengi sana kuhusu Billy Graham, hamsikii mengi kuhusu Oral Roberts. Ninaona mikutano yangu ikififia. Kuna nini? Tuko mwishoni, wakati mwingine.

82 Billy Sunday aliingiaje na hao wengine? Waliingia mara tu baada ya ufufuo wa Moody. Moody aliingia wakati gani? Mara tu baada ya ufufo wa Knox. Knox aliingia lini? Mara baada ya

ufufuo wa Finney. Finney baada ya Calvin, Calvin baada ya . . . Kwa hiyo, Wesley, naye Wesley baada ya Luther. Na kotekote katika nyakati ukaja. Mara baada ya ufufuo mmoja, kwisha, Mungu anainua mwingine na kutupa Nuru zaidi; unaendelea kwenda tu namna hiyo.

83 Sasa tuko katika mwisho wa wakati huu. Kila mtu amekutazamia Kuja kwa Kristo katika mwisho wa kipindi chake cha wakati, bali wao walikuwa na mengi sana ya kutazamia; kule kurudi kwa Wayahudi, na visahani virukavyo angani, mambo yote tunayoona siku hizi. Bali sisi tuko kwenye mwisho. Tuko hapa sasa. Wao walijua Kanisa linapaswa kupokea Nguvu ambazo zingefanya kazi katika Kanisa kazi zile zile za Kristo, kwa maana kadiri kivuli kinavyokuwa kizito zaidi na zaidi, na kurudisha zaidi.

84 Hebu chukua kivuli. Kadiri unavyokuwa mbali na hicho kivuli, ndivyo unavyopata kurudishwa kudogo sana kwa kivuli. Baada ya kitambo kidogo, kile kivuli kinazidi kuwa karibu, mpaka ule mti na kile kivuli ni kitu kile kile.

85 Sasa, Roho wa Mungu ametenda kazi chini ya kuhesabiwa haki, chini ya Luther; kutakaswa, chini ya Wesley; ubatizo wa Roho Mtakatifu, chini ya Pentekoste; na Huyu hapa katika siku ya mwisho, akitenda na kufanya mambo yale yale aliyofanya alipokuwa katika Kristo. Ni nini? Kanisa na Kristo wamekuwa kitu Kimoja.

Na mara watakaposhikamana, muungano huo wa mwisho, Hilo litaenda kupitia angani, likipiga makelele. Wesley atafufuka, Luther, na hao wengine wote kule nyuma katika siku zile kule, “yeye aliye wa kwanza atakuwa wa mwisho, yeye aliye wa mwisho atakuwa wa kwanza,” ndipo ufufuo utakuja.

86 Tuko katika wakati wa mwisho. Sikilizeni, hivyo ndivyo Roho Mtakatifu anavyofanya. Roho Mtakatifu, kwa kuhesabiwa haki, mnaona, kivuli kidogo tu Chake; Roho Mtakatifu, kwa kutakaswa, kivuli kizito zaidi Chake; Roho Mtakatifu, kwa Ubatizo Wake, kivuli kizito zaidi; sasa Roho Mtakatifu, kwa kurudishwa kwa Utu Wake kabisa kuwa humu ndani, akifanya ishara na maajabu kama alivyofanya hapo mwanzo. Whiu! Utukufu! Mtaniita “mtakatifu anayejifingirisha,” hata hivyo, afadhali muanze sasa.

87 Sikilizeni, enyi ndugu, sikilizeni jambo hili.

> *. . . meza zote zimejaa matapiko; hapana mahali* palipo pasafi.
>
> *Atamfundisha nami maarifa?* Atamjulisha, *atamfahamisha nani habari hii? wale walioachishwa maziwa, na walioondolewa matitini.*

Si watoto wachanga; watoto wachanga wa Kipresbiteri, watoto wachanga wa Kimethodisti, watoto wachanga wa

Kipentekoste, watoto wachanga wa Kiluteri, watoto wachanga wa Kinazarayo. Yeye anataka mtu fulani ambaye yuko tayari kuondoka kutoka matitini na kula chakula kigumu. Hiki hapa kinakuja:

> *Kwa maana ni amri juu ya amri,. . .juu ya amri, kanuni juu ya kanuni;. . .juu ya kanuni; huku kidogo na huku kidogo.*
>
> *La, bali kwa midomo ya watu wageni, na lugha* zingine *nitasema na watu hawa;*
>
> *Ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia.*

88 Roho Mtakatifu, kama hivyo sivyo ilivyotukia kwenye siku ya Pentekoste, alitabiriwa miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajaja! Huyu hapa kwenye siku ya Pentekoste, alikuja tu vile vile hasa.

89 Mtu fulani alisema, "Kuiadhimisha siku ya Sabato." Mimi sikatai wala kudharau kanisa ama dini ya mtu fulani. Bali kasema, "Siku ya sabato, sabato ya Mungu ilikuwa siku ya raha."

Hii *hapa* siku ya raha. [Ndugu Branham anachukua Biblia yake.] "Hii ndiyo raha," Yeye alisema, "kwamba mpeni raha yeye aliyechoka." Ndiyo hiyo. Amina! "Itakuwa amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni." Hii hapa raha. Roho Mtakatifu ni nini? Ile Raha. Loo!

> *Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*

90 Yeye ni nini? Yeye ajaye ndani yako, anakupa amani; ishara yako, Msaidizi wako; umefarijiwa, una raha, umetiwa muhuri.

91 U hali gani? Ni ishara; ulimwengu unajua kitu fulani kimetukia kwako. Yeye ni nini? Ni Mfariji. Yeye ni nini? Muhuri. Una raha. Ume-. . .Yeye ni Mwombezi wako. Kama, wewe, kitu fulani kikupate, kuna Kitu fulani kule kukuombea upesi sana, unaona, akikuombea. Ni Roho wa Mungu akiishi Kanisani, aliyetabiri itakavyokuwa hasa Yeye atakapokuja. Yeye angekuwa ishara ya milele, Raha ya milele!

92 Mungu aliufanya ulimwengu. Waebrania, sura ya 4. "Mungu aliufanya ulimwengu, kisha akapumzika katika siku ya saba." Hiyo ni kweli.

Siku ya nane ikarudi, chini. . .Yeye alitoa hiyo kwa Wayahudi kwa ajili ya agano, kwa kipindi fulani cha wakati. Hiyo ni kweli. Lakini wao wanaenda na kupumzika siku moja; wanarudi, siku ya kwanza ya juma, wanaanza tena, upya, waanza tena. Hiyo siyo raha aliyonena Mungu.

Wakati Mungu alipoufanya ulimwengu katika siku sita, alipoenda kupumzika, alipumzika tangu wakati huo na kuendelea. Hiyo ni kweli. Hilo latosha. Yeye hakurudi katika siku ya nane na kuanza tena.

93 Ilikuwa ni kivuli tu. Naam, huo ulikuwa ni mfano, kama wa mwezi kwa jua; lakini jua linapochomoza, hatuhitaji mwezi tena. Sasa angalia jambo hili, loo, katika Ufunuo 11, "Yule mwanamke aliyekuwa na mwezi chini ya miguu yake, na jua kichwani mwake." Loo, tungepitia katika Biblia, kutoka kifuniko hata kifuniko, na kuwaonyesha. Mnaona?

94 Bali ni nini? Wakati, Biblia ilisema katika Waebrania sura ya 4, "Kama Yesu angaliwapa siku ya raha, angalinena habari zake baadaye; Yeye angalinena juu ya siku ya raha." Ni siku gani Yeye alinena habari zake, raha?

> *Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha.*

95 Mathayo sura ya 11, aya ya 22. . . Angalia, basi, tunakuta kwamba tunapokuja Kwake. "Kwa maana yeye," kasema Waebrania 4, "ambaye amekwisha ingia katika raha ya Yesu, amekoma kutoka kazi zake za kilimwengu, kama Mungu alivyofanya kutoka Zake," wakati alipoufanya ulimwengu, wala hakuirudia tena! Muda gani? [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani mara tatu—Mh.] Mmetiwa muhuri kwa muda gani na Roho Mtakatifu? "Hata siku ya ukombozi wenu." Huyo hapo ile raha, faraja, Mwombezi, muhuri, Mkombozi. Loo! [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja.] Ninasisimka kwa namna fulani, ama ninabarikiwa kwa namna fulani. Loo!

96 "Ni ahadi kwetu, Ndugu Branham? Imethibitishwa na Biblia?"

Sawa, hebu tufungue Yoeli, tuone yale Yoeli aliyosema juu yake.

Jinsi ninavyoshukuru kwa ajili ya Neno lililobarikiwa la Mungu! Mnalipenda? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nafikiri ya kwamba kama isingalikuwa kwa ajili ya Neno, sijui ambako tungesimama. Sawa.

Tuko katika Yoeli sasa. Tutafungua Yoeli, sura ya 2 ya Yoeli, nasi tutaanza kwenye aya ya 28. Yoeli 2:28, miaka mia nane kabla ya kuja kwa Kristo, yule nabii katika Roho. Sasa sikilizeni.

> *Hata itakuwa* baadaye, *ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili;. . .wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono;*
>
> *Tena juu ya watumishi* wangu na juu ya watumishi wangu wanawake nitamimina katika siku hizi. . . nitamimina katika siku *hizo roho yangu.*

*Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu* za juu *na katika dunia, damu,...moto, na minara ya moshi.*

*Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya BWANA iliyo kuu... itishayo.*

*Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliitia jina la BWANA ataponywa;*

97 Hiyo ni...Loo! Nini? Yoeli! Mliona? Katika Matendo 2, Petro alichukua aya ile ile. Kasema, "Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno yangu. Hawa hawakulewa," hawa watu waliotiwa muhuri, wakafarijiwa, watu wa kipekee, waliotiwa alama. "Hawa hawakulewa, kama mnavyodhania," Matendo 2, "kwa sababu hii ni saa tatu ya mchana. Bali jambo hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, akisema, 'Itakuwa siku za mwisho kwamba nitawamwagia watu wote Roho Yangu.'"

98 Huyo ni nini, Roho Mtakatifu ni nini? Vema, sasa hebu tuone tena, aliahidiwa kwa waamini, hivyo ndivyo alivyo. Naam, Roho Mtakatifu huyu, tutaona Yeye ni nini, hebu kidogo. Ameahidiwa nani? Waamini.

Sasa hebu twende katika Luka, sura ya 24 ya Luka, na tusikize yale Yesu aliyosema katika maneno Yake ya mwisho kabla hajaondoka duniani. Luka sura ya 24. Nanyi ambao mnaandika jambo hili sasa, mnaweza kuliandika, kisha mlisome kirefu kesho wakati mna wakati mwingi zaidi. Basi, Luka 24:49, sikilizeni Yesu akinena. Hapo mwisho, alipokuwa akipaa juu Utukufuni, kule kupaa, haya hapa maneno aliyowaambia wanafunzi Wake.

*...tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu;...*

Ahadi gani? Ule Muhuri, ile ishara, yule Mfariji, na mambo haya yote ambayo nimenena juu yake, mara maelfu zaidi.

*...nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu;...*

Ahadi gani? "Ile Isaya alisema ingekuja. 'Kwa midomo midomo ya watu wageni na kwa lugha nyingine nitasema na watu hawa.' Nitatuma raha juu yenu. Nitatuma kile Yoeli alichonena, ya kwamba, 'Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia ninyi Roho Yangu.' Loo, nitawapelekea ninyi, na kuyafanya mataifa yote, watu wate, kuanzia Yerusalemu...Nitamwingiza mzao wa Ibrahimu chini ya agano hili. Nitamtia muhuri kila mmoja wao. Mnaona, nitaimwaga Roho Yangu."

...Mimi *nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu; lakini kaeni,* linamaanisha, ngojeni *lakini kaeni* mjini Yerusalemu *hata* mtakapovikwa *uwezo utokao juu.*

99 Roho Mtakatifu ni nini basi? “Nguvu zitokazo Juu!” Si nguvu zitokazo kwa askofu, si nguvu zitokazo kanisani. Bali, “Nguvu zitokazo juu!”

100 Nguvu hizo zilikujaje? Kwa “kujiunga na kanisa”? Ninawasai kufanya hivyo, kusema ya kwamba hiyo ni kweli. Kwa “kujiunga na kanisa, kupeana mikono na mhubiri”? La, bwana. Naam, kwenu ninyi Wakatoliki, “huku mkitoa ulimi wenu na kushiriki ushirika”? La, bwana!

101 Zilikujaje, Nguvu zitokazo Juu? Hebu tusome mbele zaidi. Hebu twende katika Matendo 1:8. Wao wanakusanyika pamoja sasa. Sasa wao walikuwa wanazungumza juu ya Yesu hapa, walipokuwa wamekusanyika pamoja, nao walikuwa wamemchagua mwingine kupachukua ma-—mahali pa Yuda. Matendo 1:8:

> *Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu* huyu *Roho Mtakatifu;. . .*

Nini? “Mnakuwa washiriki wa Maskani ya Branham”? La! “Mnakuwa wafuasi wa kanisa la Kimethodisti, kanisa Katoliki, la Kipresbiteri”? Sivyo, katika Biblia. Hilo ni fundisho la kujibunia.

“Lakini utapokea nguvu ukiisha kuwa mhubiri!” La, bwana! “Utapokea nguvu ukiisha kupata Shahada ya Sanaa”? La, bwana “Utapo-. . . .nguvu zitakuja ukiisha pata DD. yako”? La, bwana! “Utapokea Nguvu ukiisha kubatizwa katika maji”? La, bwana. “Utapokea Nguvu baada ya kupata ushirika wa kwanza”? La, bwana! Mnaona, huo wote ni upuzi wa kujibunia.

102 Sikilizeni yale Biblia iliyosema, yale aliyosema Yesu:

> *. . .mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu;. . .* (Roho Mtakatifu ni nini? Nguvu) halafu baada ya jambo hili, ninyi *mtakuwa mashahidi. . .* (“Ninyi kumi na wawili tu, enyi mashahidi huko Yerusalemu”?). . . ninyi *mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu,. . .Uyahudi. . . Samaria, na hata* pande za mwisho *za nchi.* (Ambazo hazijafikiwa bado.)
>
> *Akiisha kusema hayo. . .akiisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea machoni pao.*

103 Naam, fungueni ukurasa unaofuata, angalieni nabii hizi zikitimia.

> *Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako mahali. . .walikuwako wote* katika moyo mmoja *mahali pamoja.*

“Na kwa ghafula mchungaji akaja na. . .”? Nimeenda kombo hapo, sivyo? “Kwa ghafula kasisi akaja madhabahuni”? La.

> *Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi. . .*

Si kuigiza tu; Huo ulikuwako, uvumi.

"Muhudumu alikuwa anakaribia mlango"? "Kasisi alikuwa na ushirika, akitoka katika mahali patakatifu"? La, hakuna kitu kama hicho.

> . . .*kukaja ghafula toka mbinguni uvumi* . . .(Si mchakacho wa miguu). . . *Kukaja ghafula toka mbinguni uvumi wa*. . .*nguvu ukienda kasi,*. . . (loo, jamani! Whuushi. . .?. . .). . .*ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.*

104 Roho Mtakatifu ni nini? Hapa ndipo wanapopata Nguvu. Hapa ndipo wanapopaswa kungoja; hivi ndivyo ilivyotukia walipongoja. Wote walitabiri, kutoka Mwanzo moja kwa moja mpaka, kutoka Ibrahimu moja kwa moja na kuendelea; Huyo angekuja, na jinsi angekuja, na matokeo yake. Ni nini? Aliahidiwa Kanisa, kwa waamini.

> . . .*ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi.*
>
> *Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama*. . .*za moto uliowakalia kila mmoja wao.*
>
> *Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka.*

Sasa, tutafikia jambo hilo, Ijumaa usiku. Tutaliacha hilo papo hapo, mnaona?

105 Akoje? Ameahidiwa Kanisa, ahadi kwelikweli. Vema!

106 Naam, sasa tutatambua, baada ya wao kujazwa, walitiwa muhuri kwa muda gani? [Kusanyiko linasema, "Hata siku ya ukombozi."—Mh.]

Ni wangapi hapa walio na Roho Mtakatifu? Hebu tuone mikono yenu. Kuna wengi walio na Roho Mtakatifu kuliko wasio Naye. Tunataka wewe uwe mmoja wetu, ndugu, dada. Unapofahamu Yeye ni nini, Yeye ni. . . Yeye ni Roho wa Mungu anayekaa ndani yako, kufanya kazi za Mungu.

Wakati Mungu alipowahi kutuma cho chote cha Roho Mtakatifu katika ye yote wa watumishi Wake, ye yote wa manabii Wake, ye yote wa waalimu Wake, ye yote wa mitume Wake, wao daima walikataliwa na ulimwengu. Walidhaniwa kuwa wana kichaa, katika kila wakati uliokuweko. Hata wakati Paulo aliposimama mbele ya Agripa, alisema, "Kwa njia ile waiitayo uzushi. . ." *Uzushi* ni nini? "Kichaa." "Katika njia waiitayo kichaa, kundi la nati, hivyo ndivyo ninavyomwabudu Mungu wa Baba zetu." [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.] Ninafurahi sana ya kwamba naweza kusema mimi ni mmoja wao. Naam, bwana. Hiyo ni kweli. Ninafurahi sana naweza kusema mimi ni mmoja wao.

107 Naam, baada ya huyu Roho Mtakatifu kuwashukia, aliwafanya wapenzi sana, hata kila kitu kilikuwa katika shirika.

Sivyo? Jamani, jamani, ni ushirika wa namna gani! Tunauimba wimbo huo wakati mwingine: “Loo, ni ushirika wa namna gani! Loo, ni furaha ya Kiungu ya jinsi gani!” Ndivyo ilivyo. Wao hawakujali, hawakujali iwapo ju—jua liliangaza ama halikuangaza. Wao hawakuomba wapate kitanda rahisi cha maua.

“Naam, nitampokea Roho Mtakatifu,” baadhi ya watu huniambia, “Bw. Branham, kama ungenihakikishia ya kwamba nitakuwa milionea, kama utanihakikishia nitapata visima vya mafuta, na nitapata migodi ya dhahabu, na ni—ni . . . ” Mnaona, watu wanafundisha hayo, nao wanafundisha uongo. Mungu hajaahidi vitu hivyo.

108 Mtu ambaye amempokea Roho Mtakatifu hajali kama ataomba chakula, ama hataomba. Haileti tofauti yo yote kwake. yeye ni kiumbe kinachoelekea Mbinguni. Yeye hana . . . Hana mambo yanayomfunga hapa, kamwe. Hiyo ni kweli. Hajali. Yaje, yaende, yo yote yale. Acha walaumu, wafanye mizaha. Upoteze sifa zako, unajali nini? Uko njiani ukienda zako Utukufuni! Haleluya! Macho yako yameelekezwa kwa Kristo, nawe unaenda zako. Hujali ulimwengu unasema nini.

Hivyo ndivyo alivyo Roho Mtakatifu. Yeye ni Nguvu, Yeye ni muhuri, Yeye ni Mfariji, Yeye ni Mwombezi, Yeye ni Ishara. Loo, jamani! Ni dhamana kwamba Mungu amekupokea.

Nimechukua muda gani? Nina dakika nane tu zaidi. Vema. Hebu mimi . . . Nina Maandiko mengi sana hapa. Sifikiri ninaweza kuyaingiza, bali tuta—tutajaribu vyema tuwezavyo.

109 Naam, mtu akiisha kujazwa na Roho Mtakatifu, inawezekana kwamba mateso na kadhalika yangemfanya arudi nyuma na . . . Naam, yeye hatapotea; yeye angali ni mwana wa Mungu, atakuwa hivyo daima, kwa maana umetiwa muhuri kwa muda gani? [Kusanyiko linajibu, “Hata siku ya ukombozi”—Mh.] Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo ilivyosema Biblia.

110 Naam, baada ya wanafunzi kupigwa, walikuwa wamedhihakiwa, wakafanyiwa mzaha, na kila kitu, walifikiri wakati umefika wa kurudi nyuma muda kidogo. Hebu tufungue katika—katika Matendo sura ya 4, na tuone wakati wao . . . kile kilichotukia. Sasa hii ni kwenu enyi watu ambao tayari mmempokea Yeye. Matendo sura ya 4.

Basi, Petro na Yohana walikuwa wamepigwa, wakafungwa gerezani, kwa ajili ya kuponya, kufanya ibada ya kuponya kule nje kwenye lango la kanisa. Wangapi wanajua jambo hilo? Kulikuwako na mtu aliyekuwa amelala pale, kwa namna fulani amelemaa miguuni mwake. Asingeweza kutembea; alikuwa namna hiyo kwa muda wa miaka arobaini. Basi Petro akapita pale. Naye akasema . . . akainua kofia yake, apate kitu cha kuweka kwenye kofia yake, kwa ajili ya chakula.

Naye Petro akaonyesha ya kwamba alikuwa mhubiri aliyejazwa na Roho Mtakatifu, hakuwa na pesa yo yote. Yeye alisema—alisema, "Sina fedha wala dhahabu." Mnaona, yeye hakuwa anajali jambo hilo. Bali alikuwa ki—kiumbe anayeelekea Mbinguni. Loo, laiti tungalikuwa na wakati wa kukaa katika jambo hilo kwa muda kidogo pale, mnaona. Yeye alikuwa anaelekea Mbinguni. Alikuwa amefarijiwa. Alikuwa na Roho. Alikuwa na Nguvu. Aliendelea mbele akasema, "Sina fedha wala dhahabu, bali nilicho nacho nitakupa."

Hapana shaka mtu huyo alisema, "Una nini, Bwana?"

"Nina imani. Nina kitu moyoni mwangu kilichoanza kama siku kumi zilizopita. Nilikuwa kwenye chumba cha juu kule, na kwa ghafula, ahadi zote ambazo Mungu alikuwa ametoa . . . Nilikuwa nimetembea pamoja na Yesu Kristo kwa miaka mitatu na nusu. Nilitega Naye samaki, kule nje nikivua samaki. Nilifanya mambo haya mbalimbali. Nami nilikuwa nimemwona akiwaponya wagonjwa. Ni . . . aliendelea kuniambia, 'Baba yumo ndani Yangu; bali nitakapoondoka, Yeye atakuja ndani yenu.' Kwa hiyo, nisingeweza kufahamu jambo hilo. Bali Yeye alisema, 'Naam, siwatarajii kufahamu jambo hilo.'"

Hufahamu mambo haya; unayapata tu.'" Mimi silifahamu bado. Nawe usiniambie unalifahamu; kwa sababu, hulifahamu. Unaona? Kwa hiyo, siwezi kufahamu jambo Hilo, siwezi kulielezea; bali jambo ninalojua tu, ninaye Huyo.

"Vema, vema," unasema tu, "hilo si la kisayansi." Loo, bila shaka ni la kisayansi.

111 Ziangalie nuru hizo. Wakati Benjamin Franklin alipoipata, alisema, "Nimeipata." Yeye hakujua alichokuwa amepata, bali alikuwa ameipata. Nami nataka mtu fulani aniambie usiku wa leo nguvu za umeme ni kitu gani. Wao hawajui bado ni kitu gani, bali tunayo. Amina. Hiyo ni kweli. Hakuna mtu anayejua nguvu za umeme ni kitu gani. Wao wanaweza kuzitumia, kuzifanya ziwashe, kuzifanya ziwake, kuzifanya zitende. Bali zina—zinafanyizwa na jenereta, vipande viwili vikifanya kazi pamoja namna *hiyo*. Inatoa hizo, na hilo ndilo tu yote wanayojua. Zitatoa nuru, na zina nguvu ndani yake.

112 Na jambo hilo ni kama Roho wa Mungu. Unapompata kipande kimoja, ni wewe, na kipande kile kingine ni Mungu; kisha unavifanya vifanye kazi pamoja namna *hiyo*, atakufanyia kitu fulani. Hiyo ni kweli! Atatoa Nuru. Atatoa Nguvu. Hujui ni kitu gani, wala kamwe hutajua ni kitu gani, bali unajua ukiwa Naye. Hilo ni jambo moja la hakika. Basi ni kwa ajili yako. Ni wako. Ni dhamana. Hiyo ni kweli.

Nuru *hiyo* inayonyesha nini? Kuna hakikisho. Ni nuru.

Sasa angalia jambo hili. Naam, hujui ni nini.

113 Lakini watu hawa walisema, "Vema," wao wange-... wao walisema jambo moja walilojua, "tunajua ya kwamba ninyi hamna elimu." "Nati" zingine, mnaona, kama maskini yule Mjerumani alivyosema alikuwa. Mnaona? Kasema, "Wao hawana elimu wala hawana maarifa. Bali wamekuwa pamoja na Mvuvi yule, Seremala yule kule chini, aitwaye Yesu, Nitawaambia, kwa maana wao wanafanya jambo lile lile analofanya Yeye."

114 Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, ni Yesu akiishi katika mvuvi asiye na elimu, seremala, ama cho chote kile, mhubiri asiye na elimu, cho chote kile. Ni mtu anayetaka kuwa mjinga kwa mambo ya ulimwengu, na kumwacha yule Yesu aingie ndani yake, Roho wa Mungu, ule Mhuri, yule Mfariji. Yeye hajali juu ya sifa; kitu anachotaka tu ni Mungu.

115 Wakati Mungu alipokuwa akiweka katika taratibu, Yeye alisema, "Ninyi Walawi wote, nimewaita na kuwafanya makuhani. Na ndugu zenu wote, hao wengine, wale makabila kumi na mawili na siyo...hao makabila mengine kumi na moja watawatolea zaka."

"Wakati, unapopata pishi tisa za matofaa, mwaga pishi moja kwa ajili ya Walawi. Unapowapisha kondoo zako u—ukumbini hapa, chukua kondoo wa kumi. Sijali kama ni mdogo, ama mkubwa, mnene, ama ni mbaya, huyo ni wa Walawi.

"Naam, enyi Walawi, mnapopata hivi vyote, basi mtoe zaka, pia, kwa Bwana." Mnatoa sadaka ya kutikisa, sadaka za kuinuliwa, sadaka mbalimbali. Mumtolee Bwana zaka.

116 Kasema, "Musa, sehemu yako, Mimi ni wako." Loo, jamani! Akasema, "Mimi ndimi sehemu yako iridhishayo."

Na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo kwa Kanisa leo. Fedha na dhahabu sina, bali nina Sehemu iridhishayo. Haleluya! Elimu, ni vigumu kwangu kusoma Kitabu hiki, bali nina Sehemu iridhishayo. Hilo ni nzuri. Digrii ya Udaktari, sina yo yote; Ma Ph.D, ma LD, wala cho chote kile. Bali kuna kitu kimoja nilicho nacho, Sehemu iridhishayo. Hiyo ndiyo sehemu ninayotaka. Hiyo ndiyo sehemu Mungu anataka uwe nayo. Tupilia mbali vitu hivi vingine, sifa zote na cho chote kile, kisha utoke nje, ukapate Sehemu ya Mungu iridhishayo.

117 Maana ulicho nacho cha dunia hii, utakiacha hapa utakapoondoka. Bali kama una Sehemu hiyo iridhishayo, itakunyakua juu bila shaka. Daima tunachukua bima, siku hizi, kumpa mzishi. Hebu tupate Sehemu ya Mungu iridhishayo, kisha tumpate Mnyakuaji badala ya mzishi. Mwajua, wote wawili wanafanya kazi.

118 Naam, hebu tuone.

*...walipowafungulia, wakaenda kwa watu wao,...*

Si kurudi kwa makuhani. Mnaona, hiyo ilionyesha ya kwamba walikuwa Naye. Hawakuwa wakirudi kwenye kitu hicho cha kale, baridi, na cha kawaida tena, la; kurudi na kusema, "Sasa angalieni hapa yale waliyotutendea!" La, la. Wao walikuwa na kundi lao wenyewe. Kulikuwako na kama dazani moja tu yao kule, bali hilo lilikuwa kundi la kutosha, kundi ndogo sana la watu.

> . . . *walipowafungulia, . . .*

Baada ya kuwapiga na kuwatisha, kasema, "Kama mkibatiza kamwe katika Jina la Yesu tena!" Ama, loo, nilimaanisha nini hii . . . Vema, hiyo ni kweli. Mnaona? "Kama mkihubiri kamwe katika Jina la Yesu tena, hata mfaye nini, tutawapata!"

119 Kasema, "Whiu, hilo ni tisho kweli. Hebu twendeni kwa hao ndugu wengine." Loo, hiyo ndiyo njia. Katika umoja kuna nguvu. Katika umoja kuna nguvu. Kasema, "Hebu twendeni kule kwa ndugu wengine tuone tunaloweza kufanya."

120 Basi wote wakakusanyika na walikuwa wakisimulia matukio mbalimbali.

> . . . *walipowafungulia, wakaenda kwa watu wao, wakawapasha habari ya mambo yote waliyoambiwa na wakuu wa makuhani na wazee.*
>
> *Nao waliposikia, wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, . . .*

Naam, sikilizeni waliyosema. Waangalieni, waangalieni, si kurudi na kusema, loo, kitu fulani juu ya, "Ee, Bwana, ninasikitika . . ." La. Wao tayari walikuwa wameokoka. Walikuwa wamejazwa na Roho. Walikuwa na Uzima wa Milele.

> . . . *wakampazia Mungu sauti zao kwa moyo mmoja, wakisema, Mola, wewe ndiwe Mungu, . . .*

Amina! Ninapenda tu hilo, Ndugu Palmer. Ninapenda hilo.

> . . . *wewe Mungu,* (tunajua jambo hilo) . . . *ndiwe uliyefanya mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo;*
>
> *Nawe ulinena kwa Roho Mtakatifu kwa kinywa cha Daudi, mtumishi wako, . . .*

121 Sasa angalia, utarudi, useme, "Naam sisi si . . ." Sasa unaenda kule na kusema, "Vema, sasa, Bwana, sasa ngoja kidogo hapa. Wao wananifanyia tu mzaha mwingi!" Hivi Yeye hakusema wangefanya hivyo?

"Wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa."

"Vema, mwajua, bosi wangu aliniambia kama akinishika . . ." Hivi wao hawakusema wangesema jambo hilo?

"Vema, mwajua, walinipeleka mahakamani juzijuzi, juu ya jambo Hilo."

122 Hivi Yeye hakusema, "Mtaletwa mbele ya wafalme na watawala, kwa ajili ya Jina Langu. "Msifikiri-fikiri mtakavyosema, kwa kuwa si ninyi msemao"? Niliona jambo hilo likitendeka jana. "Ni Roho Mtakatifu anayekaa ndani yenu; Ndiye atakayenena." Mnaona, "Yeye." Hiyo ni kweli. Vema. "Msifikiri-fikiri mtakayosema."

> Mola, kwa. . .*Nawe ulinena kwa kinywa cha. . . Daudi, mtumishi wako,* amesema, *Mbona* makafiri *wamefanya ghasia, na makabila wametafakari* jambo la *ubatili?*
>
> *Wafalme wa dunia wamejipanga, na wakuu wamefanya shauri pamoja juu ya Bwana na juu ya Kristo wake.*
>
> . . .*ni kweli,* Bwana, *Herode na Pontio Pilato pamoja na Mataifa na watu wa Israeli,. . .likusanyika katika mji huu juu ya Mtumishi wako mtakatifu Yesu, uliyemtia mafuta,*
>
> *Ili wafanye yote ambayo mkono wako na mashauri yako yamekusudia tangu zamani yatokee.*

Loo, jamani! Ninapenda jambo hilo. "Bwana, wao wanafanya tu jambo lile lile Wewe ulisema wangefanya." Biblia ingesemaje?

> "Katika siku za mwisho, watakuja watu wenye kudhihaki, *wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu;*
>
> . . .*wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji. . . wasiopenda mema,*
>
> *Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana. . . .*

Wao hawakupanda kule juu na kupokea Nguvu, "baada ya Roho Mtakatifu kuja juu yenu."

> *Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana nguvu zake; hao nao ujiepushe nao."*

Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo. Mnaona?

> . . .yale *yaliyokusudiwa kufanywa.*
>
> . . .*sasa, Bwana, yaangalie matisho yao; ukawajalie watumwa wako kunena Neno lako kwa ujasiri wote,*

Loo, napenda jambo hilo! Ondoa huo mfupa hafifu, upate uti wa mgongo halisi mle ndani. Sasa angalia hapa.

> . . .*kunena kwa maneno ya ujasiri,*
>
> *Ukionyosha mkono wako kuponya;. . .*

Loo, Ndugu! Pepo hawafi, lakini Roho Mtakatifu hafi pia. Mnaona?

> . . . *ukiunyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la mtumishi wako mtakatifu Yesu.*

Mnaona kile wanachozozania, sivyo? Wao wanafanya jambo lile lile leo, bali haliwasaidii hata kidogo.

> *Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.*

123 Whiu! Jamani! Wao walipata kitu fulani walipopanda kule, sivyo? Ile ahadi ilisema ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, kukupa ujasiri, kukupa faraja, kukutia muhuri, kukupa ishara. Loo, jamani!

124 Sikilizeni. Loo, laiti tungalikuwa tu na wakati, tungeshuka pamoja na Filipo kwenda kwa Wasamaria. Katika Matendo 8:14; ninyi nyote mnaoyaandika. Wao walikuwa wamepokea furaha kuu, waliisha kuwa na kuponya kwingi, bali walikuwa wamebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Lakini wakatuma Yerusalemu, kumleta Petro; akashuka akaja akawawekelea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Matendo 8:14.

125 Mataifa, kulikuwa na mmoja jina lake Kornelio. Yeye alikuwa mtu mzuri sana, alitoa zaka, akawajengea watu masinagogi, alimheshimu Mungu, alimcha Mungu; mtu mzuri, Mpresbiteri mzuri, Mmethodisti, Mbatisti, ama cho chote kile, mnaona, mtu mzuri sana. Lakini siku moja, Mungu akasema, "Yeye ni mtu mzuri; kwa hiyo nitamtuma tu kwenye mkutano fulani. Itanibidi kumpeleka mhubiri wangu kule kumwambia juu ya jambo Hilo." Vema.

Kwa hiyo akaona ono, likasema, "Shuka uende Yafa, nawe utampata mtu mmoja kule jina lake Simoni, mtengenezaji wa ngozi. Na kuna mmoja, Simoni Petro, kule ndani. Hebu aje hapa; atakwambia ile njia, maana yeye amepokea kitu fulani."

126 Basi Petro alipokuwa amesimama kule juu . . . Naye Kornelio alikuwa anataka kumwabudu mhubiri huyo. Alikuwa anataka. Lakini Petro akasema, "Simama. Mimi nami ni mwanadamu kama ulivyo wewe."

"Basi Petro alipokuwa akisema Maneno haya," jinsi walivyorudi nyuma, hapo mwanzo kwenye . . . Mambo yale yale ninayonena habari zake, jinsi Mungu alivyoahidi kumwaga Roh Mtakatifu. "Alipokuwa akinena Maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia." Whiu! Naam. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo, kwamba ni wa nani. Hakika. "Nao wote wakajazwa na Roho Mtakatifu."

127 Sasa angalia katika Waefeso, kulikuweko na Ndugu wa Kibatisti. Yeye kwanza alikuwa mwana-sheria, mwerevu, mtu mwenye akili, alijua torati; mtu mashuhuri, mwanachuoni. Siku moja alianza kusoma Biblia, akaona ya kwamba mtu

mmoja angekuja kwa jina la Masihi. Basi alipofanya hivyo, mbona, akaanza kusikia habari za Yesu huyu, ndipo akasema, “Mimi nimeshawishika. Nami naungama hadharani imani yangu kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu.” Yeye alikuwa Mbatisti halisi. Huyu hapa anakuja moja kwa moja, “Nakiri hadharani ya kwamba Yesu ndiye Kristo.” Aliendelea kufanya jambo hilo sana hata Mungu akamwita katika huduma. Mungu daima atanena na moyo wa kweli.

128 Basi kulikuwako na maskini fundi mzee wa kushona hema kule chini jina lake Akila na Prisila, mume na mke. Wao walikuwa fundi wa kushona hema. Matendo sura ya 18, inakwambia habari hizo. Paulo, wao walikuwa marafiki wake. Wao walikuwa wamempokea Roho Mtakatifu chini ya mikono ya Paulo na mafundisho yake.

Wakasikia kulikuwako na ufufuo kule, kwa hiyo wakaenda kule. Kulikuweko na kumi ama kumi na wawili waliouhudhuria. Kwa hiyo akaenda kule kuangalia jambo hilo, ndipo akamsikia huyu mhubiri akihubiri, kwa ukujufu wa moyo wake. Akasema, “Mwajua, ninaamini yeye angesikiza Kweli.”

Kwa hiyo ibada ilipokwisha, alimwita karibu na hema, akasema, “Angalia, tuna ndugu mdogo namna hii, maskini Myahudi mwenye pua kama ndoana, na, lakini atakapokuja huku, atakufundisha Neno la Mungu, kwa udhahiri.” Vema, baada ya kitambo kidogo . . .

129 Paulo alikuwa gerezani wakati uo huo. Mahali pabaya sana kwa mhubiri wa kisasa, sivyo? Bali alikuwa gerezani, na Bwana aliacha awe mle. Kwa hiyo baada ya lile tetemeko la nchi kutokea, likaitikisa gereza sana, alimchukua mlinzi wa gereza pamoja na nyumba yake na kuwabatiza wote, katika Jina la Bwana Yesu, kisha akaondoka, akaja huku.

Naye ndiyo kwanza atoe pepo katika maskini msichana mdogo aliyekuwa anaagua. Halafu, basi, wao walikuwa wakipata fedha nyingi sana kwake, kwa hiyo alifichua tu jama zao, basi wakamfunga gerezani kwa sababu hiyo. Ndipo Bwana akaitikisa ile gereza sana, kwa kuwa Yeye alikuwa na kundi la watu kule kusikia Kweli. Huwezi kulifunga Neno la Mungu. Kuna . . . haidhuru ufanye nini, huwezi kamwe. Huwezi kufanya jambo hilo.

130 Kwa hiyo akaja kule ambako mtu huyu alikuwa. Basi Akila na Prisila, labda walikuwa na sambusa chache. Na mara baada ya kula hizo sambusa, kasema, “Tutaenda kule kwenye ufufuo.”

Paulo akaketi kule nyuma huku ameshikilia vasi lake dogo, akamsikiliza mhubiri huyu wa Kibatisti akihubiri.

Kasema, “Hayo ni sawa uliyohubiri, bali kuna mengi zaidi ya Hayo.” Kasema, “Nataka kukuuliza swali, Dk. Apolo. Je! umempokea Roho Mtakatifu tangu ulipoamini?”

"Loo," akasema, "hatujui kama alikuweko. Unamaanisha nini, na 'Roho Mtakatifu'? Sisi ni Wabatisti."

Kasema, "Mnajuaje ninyi ni Wabatisti?" Mnaona?

"Vema, tulibatizwa. Tunajua tu ule ubatizo wa Yohana."

Akasema, "Yeye alibatiza tu kwa toba, akisema 'mwamini Yeye ajaye,' huyo ni Yesu Kristo."

Basi aliposikia jambo hili, wao wakabatizwa tena, katika Jina la Yesu Kristo. Ndipo Paulo akaweka mikono yake juu yao, naye Roho Mtakatifu akawashukia, nao wakanena katika lugha na kutabiri. Kasema, "ye yote," sasa.

131 Sasa tunafanyaje jambo hilo? Nataka kuwaambieni jambo fulani, kisha ni-. . . Tutafunga, maana, ni, niliwaambia ningewaruhusu mfumukane mapema. Mnajua Roho Mtakatifu ni nini. Kwa kuwa Maandiko ya mwisho usiku huu. . . Nina kundi lingine hapa chini, bali itatubidi kuacha hayo. Hebu tufungue katika Wakorintho wa Kwanza 12. Halafu basi tutasoma hili, kisha tuta—tutafunga. Vema. Wakorintho wa Kwanza sura ya 12.

Ni wangapi wanaamini mafundisho ya Mt. Paulo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika! Yeye alisema, katika Wagalatia 1:8, "Kama Malaika alifundisha jambo lo lote tofauti, na alaaniwe," sebuse mhubiri. "Kama Malaika kutoka Mbinguni akishuka na kufundisha lo lote tofauti, na alaaniwe." Unaona, usiwe na uhusiano wo wote na jambo hilo.

132 Sasa angalia hili, Wakorintho wa Kwanza 12. Ni wangapi—ni wangapi wanajua ya kwamba hatuna budi kuwa katika Kristo kusudi tupate kufufuliwa, kwa maana Mwili Wake ndio Mungu alioahidi kuuinua? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakuna njia nyingine. Hakuna njia nyingine, kama wewe uko nje ya Kristo.

Huenda ukaangalia *huku* nyuma na kumwamini Yeye, useme, "Hakika, ninamwamini Yeye. Yeye ni Mwana wa Mungu." Sawa, ndugu yangu, niko tayari kukupa mkono unaposema hivyo. "Namwamini Yeye. Nitamkiri kama Mwokozi wangu." Hilo ni sawa, bali ungali hauko ndani Yake. "Nitampa mkono mhubiri. Nitatubu dhambi zangu." Hiyo ingali si kuwa ndani Yake.

133 Sasa angalia, angalia alilosema Paulo, jinsi unavyoingia katika Kristo. Utajulikanaje kama mtu aliyetahiriwa, Ibranimu? Walitoa ishara. Sikilizeni jambo hili sasa, Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12, na tuanzie kwenye aya ya 12:

> *Maana kama vile mwili ni mmoja, nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja; vivyo hivyo na Kristo.* (Hajagawanywa. "Mmoja!")

Sikilizeni. "Kwa maana kwa kanisa moja"? Ni wangapi wanaosoma nyuma yangu? "kwa kupeana mkono kumoja"? 'Kwa maji moja"? La. Basi mtu fulani amekosea.

"Kwa Roho mmoja!" Hiyo ni herufi kubwa? Huyo ni, "Roho Mtakatifu," basi. Mnaona?

> *. . .katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi tulinyweshwa Roho mmoja.*

134 Mwili wa Kristo ni Roho Mmoja, ambapo kila mshiriki, tangu Pentekoste hata wakati huu, hunywa Divai ile ile Mpya, Roho Mtakatifu yule yule, akileta matokeo yale yale. Tunafanyaje jambo hilo? "Kwa Roho mmoja."

Ni mlango wa Mungu uliofunguliwa, Roho Mtakatifu. Ni nini? Yeye ni mlango wa Mungu uliofunguliwa. Yeye ni ishara. Yeye ni muhuri. Yeye ni Mfariji. Yeye ni Mwombezi. Yeye ni dhamana. Yeye ni raha. Yeye ni amani. Yeye ni wema. Yeye ni kuponya. Yeye ni Uzima. Yeye ni—Yeye ni mlango wa Mungu uliofunguliwa kwa ajili mambo haya yote. Yeye ni mlango wa Mungu uliofunguliwa kuingia kwa Kristo, ambao una . . .

Mungu alithibitisha ya kwamba alimfufua Kristo katika wafu, nao hao waliokufa katika Kristo Mungu atakuja nao katika ule ufufuo. "Msimhuzuhishe Roho Mtakatifu ambaye kwaye mlitiwa muhuri kuwa katika Kristo hata siku ya ukombozi wenu." Whiu! Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

135 Kristo ni nini? Roho Mtakatifu ni nini? Si kitu ambacho watu huchekelea. Ni kitu watu wanachochekelea; bali sivyo, kwa waamini.

Kwa asiyeamini! Laiti ningalikuwa na majuma mawili matatu, ningetaka kuchukua usiku wa kesho na kuwaambia Yeye ni nini kwa asiyeamini. Hebu niyapitie haraka, kwa muda kidogo sana. Yeye ni kitu cha kuchekelea. Yeye ni mtego. Yeye ni jiwe la kujikwaa. Yeye ni mauti. Yeye ni kutengwa Milele na Mungu. Siwezi tu kukumbuka Yeye alivyo kwa asiyeamini!

136 Kumbuka, mvua ile ile ambayo wasioamini waliifanyia mzaha, ilikuwa ndiyo mvua ile ile iliyomwokoa Nuhu pamoja na jamaa yake. Mnaona? Roho yule yule, Roho Mtakatifu ambaye watu wanamfanyia mzaha na kusema ni "kichaa, na kundi la nati, ni kuingia kichaa," Hicho ndicho kitu kile kile ambacho kitalinyakuwa Kanisa na kulitwaa juu katika siku za mwisho; kitaleta hukumu juu ya asiyeamini. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyo.

137 Heri hao . . . Hebu niseme jambo hili, katika unyofu wa moyo wangu. Heri wale wenye njaa na kiu kwa ajili Yake, maana hao watashibishwa.

138 Kesho usiku tutazungumzia juu ya vile, vile Yeye anavyofanya ajapo.

139 Basi, ni wangapi humu ndani wangetaka kumpokea Roho Mtakatifu, na wanataka mtu fulani awaombee, ili kwamba muone ile nuru?

Ujue "Huyo ni nani."

Sasa, kesho usiku, tutachukua, "kile afanyacho."

140 Halafu usiku unaofuata, ni, "jinsi ya kumpokea." Kisha tutawaita, tutawafundisha watu hapa, na kuenda moja kwa moja vyumbani na kukaa mle, kama itachukua Krismasi yote, hiyo ni kweli, mpaka Roho Mtakatifu aje. Tutamwendea kutoka kwa msingi wa akili timamu wa Kibilia. Tumwendea na kumpata kama tu vile Mungu alivyomwahidi, na jinsi Yeye alivyoshuka hapo mwanzo. Hivyo ndivyo tulivyo hapa kufanya. Mimi. . .Haileti tofauti yo yote kile cho chote kisemacho, tuna-. . .

Neno la Mungu ni . . .linachukua nafasi ya kwanza moyoni mwangu. Hiyo ni kweli. Nami nataka kile Mungu alicho nacho kwa ajili yangu. Kama kuna cha zaidi, fungua Mbingu, Bwana, maana wangu—moyo wangu umefunguliwa kwa ajili yake. Hiyo ni kweli.

141 Ni wangapi wanaomhitaji? Sasa inua mkono wako, useme, "Niombee." Sasa, wakati, mikono yenu ikiwa juu.

Baba uliye Mbinguni, tumefundisha muda mrefu. Bali Roho Wako yuko hapa. Kuna mikono iliyoinuliwa hewani sasa. Nao wanajua Yeye ni nani, wao wanajua maana ya Roho Mtakatifu. Naomba, Mungu, ya kwamba kabla mkutano huu haujamalizika, ya kwamba kila mkono ulio humu ndani utainuliwa ya kwamba wao wamempokea Yeye. Tujalie, Bwana.

142 Tunawaombea. Tunakuomba uwabariki, na uwape shauku ya moyo wao. Angalia mikono yao, Bwana. Wao wanakupenda. Wanamtaka Yeye. Wanajua hawawezi kwenda . . . Kesho usiku, kama utanisaidia, Bwana, tunaweza kuthibitisha jambo hilo katika Maandiko ya kwamba wao hawatafaulu kunyakuliwa bila Yeye. Kwa hiyo naomba, Baba, ya kwamba Wewe utawapa kuona njaa na kiu, ili kwamba waweze kujazwa. Ninawakabidhi Kwako sasa, Baba. Na, zijalie baraka hizi, tunapoomba katika Jina la Yesu. Amina.

> Nampenda, nampenda,
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

143 Nataka kusema jambo hili kabla hatujaimba tena. Ninataka kukutana na kundi la wahudumu chumbani humu, Ijumaa usiku, kabla ibada haijaanza, mnaona, Ijumaa usiku. Mimi . . .

Mnaona kile ninachojaribu kufanya? Kuonyesha Yeye ni nini, jinsi ya kumwendea Yeye na kile cha kuheshimu; ndipo wewe huji kipofu, ukipigapiga kitu fulani. Hiyo ndiyo sababu mimi sikuuliza jambo hilo usiku wa leo. Ninawatakeni mjue Yeye ni nini. Ni ahadi. Yeye ni muhuri. Yeye ni Mfariji. Yeye ni kadhalika.

Halafu, kesho usiku na usiku unaofuata, basi tutaanza papo hapo, tangu wakati huo na kuendelea, mpaka Yeye atakapokuja. Sijali itachukua muda mrefu namna gani; tutakaa hata. Usafishe moyo wako. Yeye hatammwaga kamwe katika moyo ulio mchafu. Iweni sawa, iweni tayari, Naye atatujalia jambo hilo.

Nampenda, nampenda (hebu tuinue mikono
yetu sasa)
Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Mchungaji ndiyo kwanza aseme, nasi tunakubali, ya kwamba kesho usiku tutaanza kwenye saa moja badala ya saa moja u nusu. Na jambo hilo litaniruhusu niwaruhusu mtoke kwenye saa mbili u nusu badala ya saa tatu u nusu. Mnamo saa moja u nu-. . . Mnamo saa moja, kesho usiku, ibada ya nyimbo itaanza. Nitakuwa kwenye Ujumbe wangu mnamo saa moja u nusu.

Nampenda,

Na tutoe vitambaa vyetu na kuzitikiza Kwake.

Nampenda

Hebu vunjeni utaratibu wa kawaida sasa!

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Vema, mchungaji wenu sasa, Ndugu Neville.

*Roho Mtakatifu Ni Nini?*
(*What Is The Holy Ghost?*)
16 Desemba, 1959, Jumatano jioni

*Roho Mtakatifu Alitolewa Kwa Kusudi Gani?*
(*What Was The Holy Ghost Given For?*)
17 Desemba, 1959, Alhamisi jioni

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham zilihubiriwa katika Kiingereza katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani. Kila juhudi imefanywa kuzitoa jumbe hizi kwa usahihi sana kutoka kwenye kanda za sumaku na kuziandika katika kitabu, nazo zinachapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2009.

SWAHILI

©1994 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org